**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**Dkt. SAADA MKUYA SALUM,**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO, ZANZIBAR.**

**JUNI, 2024**

## YALIYOMO

A. UTANGULIZI ........................................................................1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS – FEDHA NA MIPANGO ....2
C. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ........................................3
Ukusanyaji wa Mapato ........................................................4
Fungu F01 (Ofisi ya Rais Fedha na Mipango) ..................................6
Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali) ............................7
Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali) ..............................7
Matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango..................................8
Fungu F01 (Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango)..................................9
Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali) .............................................16
Fungu F03 (Tume ya Mipango Zanzibar) .........................................17
Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali) ............................22
Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali) ..............................24
Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali) ..............................27
D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA OFISI YA RAIS -FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2023/2024......................................................................29
Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)......................................................................29
Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).....31
Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar......................32
Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa.........................................................................33
Programu ya Uimarishaji wa Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) ........................................................................34
E. UTEKELEZAJI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS -FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2023/2024......................................................................35
Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)..............................................35
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) .............................................36

Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)........37
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ........38
Shirika la Bima (ZIC) ........40
Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)........42
MASHIRIKIANO NA TAASISI NYENGINE........43
MAFANIKIO YA YALIYOPATIKANA........44
CHANGAMOTO........45
UTATUZI WA CHANGAMOTO........45
F. MWELEKEO WA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024-2025........46
Vipaumbele vya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango........46
Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ........48
Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango. ........48
Matumizi kwa Fungu F01 ........49
Matumizi kwa fungu F02........50
Matumizi kwa fungu F03........50
Matumizi kwa Fungu F04 ........50
Matumizi kwa Fungu F05 ........51
Matumizi kwa Fungu F06 ........51
Matumizi kwa Fungu F07 ........51
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais -Fedha na Mipango kwa Mwaka 2024/2025........52
MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO 2024/2025........54
Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)........54
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ........54
Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)........55
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ........56
Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)........57
Shirika la Bima (ZIC) ........58
Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri elekezi wa kodi Zanzibar (ZIAAT)........59
G. HITIMISHO ........60
H. VIAMBATANISHO ........62

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na utulivu katika nchi yetu ambayo imetuwezesha kukutana hapa leo kwa lengo la kuwasilisha utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi) 2023/2024 na makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri na kuendelea kuimarisha uchumi, umoja na mshikamano kwa wananchi wote na tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema, hekima na busara ili matamanio ya Wazanzibari yaweze kufikiwa chini ya uongozi wake. Kadhalika, nawapongeza wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais ambao ni Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa jinsi wanavyomsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili kuleta maendeleo ya Nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa umakini na umahiri wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuendelea kushirikiana na sisi na kutuongoza katika kutekeleza vyema majukumu yetu. Vile vile, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Dimani kwa kuipitia na kuijadili mapendekezo ya awali ya bajeti hii na hatimae kuridhia iwasilishwe mbele ya Baraza lako.

4. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, shukrani zangu za dhati zimwendee Naibu Waziri, Mheshimiwa Juma Makungu Juma (MB), Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu Nd. Aboud Hassan Mwinyi, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh,

viongozi wa Taasisi zinazojitegemea na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango pamoja na watumishi wote kwa kazi nzuri ya usimamizi wa masuala ya uchumi na fedha pamoja na ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya shughuli za Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya shukurani hizo, naomba uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi Rais - Fedha na Mipango kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taarifa hii imezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021 – 2026; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 na Hotuba na Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa nyakati mbalimbali. Bajeti hii pia imezingatia malengo ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ya mwaka 2022-2026.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS – FEDHA NA MIPANGO

6. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, kibajeti inajumuisha mafungu makuu saba (7) ndani yake yanaundwa na Idara ishirini na tatu (23), Taasisi saba (7) na Ofisi tano (5) za Pemba. Malengo makubwa ya kuanzishwa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ni kusimamia Fedha za Umma kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

   i. Kusimamia Mapato ya Serikali kutoka vyanzo mbali mbali yakiwemo Mapato ya Kodi na yasiyokuwa ya Kodi, Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Mikopo ya Ndani (Hati Fungani);

   ii. Kusimamia Mali za Serikali kupitia Usimamizi wa Ununuzi, Utunzaji na Uondoaji wa Mali pamoja na Hisa katika Mashirika na Kampuni binafsi ambazo Serikali inamiliki;

iii. Kusimamia Fedha za Umma na shughuli za Uhasibu na Ukaguzi serikalini, katika jukumu hili Ofisi inasimamia Bajeti ya Serikali, usimamizi wa Hazina, huduma za uhasibu na ukaguzi wa ndani serikalini;

iv. Kusimamia Deni la Taifa (Mikopo ya Ndani na Nje) kwa kutoa ushauri na kufuatilia mwenendo na udhibiti wake;

v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera thabiti, mahiri na shirikishi za kodi na fedha;

vi. Kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha, inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii na usimamizi wa Taasisi za Huduma ndogo ndogo za fedha;

vii. Kusimamia mifumo ya Ukusanyaji na Udhibiti wa fedha za umma;

viii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia idadi ya watu na mahitaji yake;

ix. Kuratibu na kusimamia maendeleo ya uchumi kupitia sekta za Kiuchumi na kijamii;

x. Kuratibu utekelezaji wa Sera za Kisekta na kupunguza umasikini nchini;

xi. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa Takwimu Rasmi kwa Maendeleo ya Nchi; na

xii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya kitaifa na kimataifa.

## C. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

7. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Fedha na

Mipango ya Mwaka 2024/2025, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Muhtasari wa utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi, 2023/2024) kama ifuatavyo:-


8. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango utekelezaji wake umegawika katika maeneo makuu manne(4), maeneo hayo ni Mapato yanayokusanywa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango (F01), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04) na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05), utekelezaji wa matumizi yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02), Tume ya Mipango Zanzibar (F03), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05) na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (F06), utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango; na utekelezaji wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango.

**Ukusanyaji wa Mapato**

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 2,767.839 bilioni,** makadirio hayo yalikua ni ongezeko la asilimia **11** ikilinganishwa na makadirio ya **TZS 2,498.211 bilioni** ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mapato hayo yamejumuisha mapato katika mafungu ya F01, F04 na F05.

10. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2023/24, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imekusanya jumla ya **TZS 2,213.748 bilioni** sawa na asilimia **101** ya makadirio ya **TZS 2,199.108 bilioni** ni ongezeka asilimia **107** ya makusanyo ya **TZS 1,071** bilioni ya kipindi Julai – Machi Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyoonekana katika mchoro wa hapo chini:-

**Mchoro 1: Mlinganisho wa Mapato, Makadirio na Halisi kwa Kipindi cha Julai –Machi Kwa Miaka**




**Chanzo: OR-FM**

**11. Mheshimiwa Spika,** Ongezeko la mapato haya limetokana na usimamizi wa mzuri sheria za kodi, ongezeko la wageni wanaoingia nchini na mwitikio mzuri wa washirika wa maendeleo. Mgawanyo wa Mapato hayo kimafungu ni kama ifuatavyo:-

i. Fungu F01 imekusanya TZS 1,516.449 bilioni sawa na asilimia 108 ya makadirio ya TZS 1,404.034 bilioni ya kipindi cha tathmini;

ii. Fungu F04 imekusanya jumla ya TZS 0.072 bilioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya TZS 0.087 bilioni ya kipindi cha tathmini; na

iii. Fungu F05 imekusanya jumla ya TZS TZS 697.228 bilioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya 794.986 bilioni ya kipindi cha tathmini.

## Mapato Fungu F01 (Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango)

12. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Machi, 2023 Fungu F01 limekusanya jumla ya **TZS 1,516.449 bilioni** sawa na asilimia **108** ya makadirio ya **TZS 1,404.034 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mapato hayo yamejumuisha mapato ya kodi, mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na mapato yasiokuwa ya kodi. Mchanganuo wake kama ifuatavyo: -

### Mapato ya Kodi

13. **Mheshimiwa Spika,** mapato haya yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar. Katika kipindi cha Julai-Machi 2023/2024, mapato yaliyokusanywa na ZRA yamefikia **TZS 559.484 bilioni** sawa na asilimia **117** ya makadirio ya **TZS 479.178 bilioni** ya kipindi cha tathmini na ni ongezeko la asilimia **25** ikilinganishwa na makusanyo ya miezi tisa ya mwaka 2022/2023 ambayo ni **TZS 449.283 bilioni.**

14. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa upande wa Zanzibar imekusanya jumla ya **TZS 384.366 bilioni** sawa na asilimia **100** ya makadirio ya kukusanya **TZS 383.978 bilioni** ya kipindi cha tathmini na ni ongezeko la asilimia **18** ikilinganishwa na makusanyo halisi ya miezi tisa ya 2022/2023 ambayo ni **TZS 325.611 bilioni.**

### Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

15. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato kutoka kwa washirika wa Maendeleo hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TZS 504.306 bilioni** zimepatikana sawa na asilimia **106** ya makadirio ya **TZS 475.819 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

### Mapato yasiyokuwa ya kodi

16. **Mheshimiwa Spika,** mapato yasiyokuwa ya kodi, hadi kufikia Machi 2024, yamekusanywa jumla ya **TZS 67.157 bilioni** sawa na asilimia 1**08** ya makadirio ya **TZS 62.384 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

### Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)

17. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kupitia vyanzo vyake vya vibali vya utafiti, ukodishwaji ukumbi na ushauri elekezi imekusanya jumla ya **TZS 71.580 Milioni** sawa na asilimia **82** ya makadirio ya **TZS 87.294 Milioni** ya kipindi cha tathmini.

### Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)

18. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2024, Ofisi imekusanya jumla ya **TZS 697.227 bilioni** sawa na asilimia **88** ya makadirio ya **TZS 794.986 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo: -

### Mapato ya Wafanyakazi (PAYE)

19. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Ofisi ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 15.750 bilioni** na hadi kufikia Machi 2024, makusanyo halisi ni **TZS 14.000 bilioni** ambayo ni sawa na asilimia **89** ya kipindi cha tathmini na sababu ya kupungua mapato hayo kumetokana na mapato ya mwezi wa Machi, 2024 kupokelewa mwezi wa Aprili, 2024.

### Mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

20. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ilikadiria kukopa jumla ya **TZS 567.210 bilioni** hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TZS 487.790 bilioni** zimepatikana sawa na asilimia **86** ya makadirio. Kwa upande wa Mapato ya Hati Fungani **TZS 108.840 bilioni** zimepatikana sawa na asilimia **73** ya makadirio ya **TZS 150 bilioni.**

### Misaada ya Kibajeti (GBS)

21. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Ofisi ilikadiria kukusanya **TZS 35.00 bilioni** hadi kufikia Machi 2024, Ofisi imekusanya **TZS 72.966 bilioni** sawa na asilimia 208 ya kipindi cha tathmini.Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka

kwa idadi na kiwango cha uchangiaji kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### Gawio la kutoka Benki Kuu ya Tanzania

**22. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2023/24 Ofisi ilikadiria kukusanya **TZS 13.500 bilioni** na imekusanya **TZS 4.500 bilioni** sawa na asilimia **33,** hii imetokana na makadirio makubwa yaliyopangwa na Ofisi.

### Mapato Mengineyo Yasiyokuwa ya Kodi

**23. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi tisa, Ofisi ilikadiria kukusanya **TZS 13.526 bilioni** hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TZS 9.131 bilioni** zimekusanywa sawa na asilimia **68** ya kipindi cha tathmini upungufu wa makusanyo hayo unatokana na kutokukamilika kwa muongozo wa uondoaji wa mali za umma, kurejeshwa nyumba zilizopo Mji Mkongwe zilizokuwa zikimilikiwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa Shirika la Nyumba na Kubadilishwa kwa matumizi ya bohari kuwa hifadhi kuu ya chakula cha Serikali. Mchanganuo wa Mapato unaonekana katika **kiambatanisho Namba 1.**

### Matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Machi 2023/24, matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango yamefikia jumla ya **TZS 376.697 bilioni** sawa na asilimia **99** ya makadirio ya **TZS 379.045 bilioni** katika kipindi cha tathmini na asilimia **55** ya makadirio ya **TZS 682.997 bilioni** kwa mwaka. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo kama ifuatavyo: -

i. Matumizi ya mishahara TZS 105.391 bilioni;

ii. Matumizi ya uendeshaji wa mafungu ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango TZS 15.971 bilioni;

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 214.955 bilioni;

iv. Ruzuku zilizopatiwa Taasisi za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango TZS 29.076 bilioni; na

v. Matumizi ya miradi ya maendeleo TZS 11.302 bilioni (ambapo TZS 6.568 bilioni zimetoka Serikalini na TZS 4.734 bilioni zimetoka kwa Washirika wa Maendeleo).

25. **Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa utekelezaji wa bajeti kwa mafungu yaliyopo Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ni kama ifuatavyo:

**Fungu F01 (Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango)**

26. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu F01, yamejumuisha programu kuu tatu (3) ndani yake zinajumuisha programu ndogo tisa(9). Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024; Fungu hili limetumia **TZS 141.531 bilioni** sawa na asilimia **94** ya makadirio ya **TZS 150.712 bilioni** katika kipindi cha tathmini na asilimia **36** ya makadirio ya kutumia **TZS 388.773 bilioni** kwa mwaka. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: -

***PF 0101-Programu Kuu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma***

27. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2024, programu hii imetumia **TZS 116.222 bilioni** sawa na asilimia **99** ya makadirio ya **TZS 117.894 bilioni** ya kipindi cha tathmini na asilimia **92** ya makadirio ya **TZS 126.703 bilioni** kwa mwaka. Programu hii imejumuisha programu ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali imetumia jumla ya TZS 86.977 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 87.015 bilioni ya kipindi cha tathmini;

ii. Programu ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje imetumia TZS 1.481 bilioni sawa na asilimia 211 ya makadirio ya TZS 703.695 milioni ya kipindi cha tathmini. Sababu iliyopelekea kuongezeka kwa matumizi katika programu ndogo hii ni gharama za kufanyika kwa Mkutano wa Tathmini ya Muda wa Kati wa Mzunguko wa 20 (IDA 20 MID-TERM REVIEW) uliofanyika mwezi Disemba hapa Zanzibar; na

iii. Programu ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi imetumia TZS 27.763 bilioni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya TZS 30.175 bilioni ya kipindi cha tathmini. Fedha hizi zimejumuisha ruzuku za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ambazo ni TZS 27.445 bilioni (Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) TZS 21.469 bilioni na Mfuko wa Barabara (ZRF) TZS 5.976 bilioni).

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Ofisi imeweza kuratibu Mkutano wa Tathmini ya Muda wa Kati wa Mzunguko wa 20 (IDA 20 MID-TERM REVIEW) uliofanyika kwa mara ya kwanza Tanzania. Mkutano huo ulilenga kutathmini maendeleo yaliyopatikana kuhusu sera na ahadi za kifedha katika Mzunguko wa 20 wa Taasisi ya Maendeleo ya Benki ya Dunia (IDA) na kutathmini muitikio wa IDA kwa Washirika wake mbalimbali. Katika mkutano huo, USD 93 bilioni ziliidhinishwa kwa ajili ya kusaidia mataifa maskini zaidi duniani ili kuimarisha maendeleo ya kijamii, kibinaadamu na kiuchumi katika mataifa hayo;

ii. Kushiriki Mkutano wa Mazingira wa 28 (COP28) nchini Dubai ambapo Tanzania inatarajiwa kunufaika na ufadhili wa USD 100 milioni kutoka kwa Bill Gate, USD 114 milioni kutoka USA, USD 44 milioni kutoka Belgium, USD 100 milion kutoka UAE; kwa ajili ya kutatua changamoto zinazotokana na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabia Nchi;

iii. Kushiriki katika kuwasilisha mkataba wa mradi wa “Tanzania Food System Resilience Programme” utakaotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Misitu chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia;

iv. Kushiriki katika kazi ya kuchambua uhimilivu wa Deni la Taifa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Zanzibar iliwasilisha taarifa zake katika zoezi hilo na kuonekana bado inakopesheka;

v. Ofisi ilishiriki mkutano wa kujadili maeneo mapya ya mashirikiano kati ya Tanzania na Kuwait ambapo Zanzibar inatarajiwa kunufaika na miradi mbalimbali ya kimkakati;

vi. Ofisi ilishiriki katika Mkutano wa saba wa mawaziri wa ushirikiano wa Fedha na Uchumi kati ya Korea na Afrika ambao Zanzibar ilinufaika kwa kukubalika kwa ufadhili wa mradi wa Hospital ya Binguni wenye thamani ya Dola za Kimarekani million 167 na mradi wa Kumbi za Mikutano wenye thamani ya USD million 92;

vii. Kushiriki katika ziara ya utafutaji rasilimali fedha kwa mradi wa maji nchini Japan ambapo Zanzibar itanufaika na mradi wa usambazaji maji mjini wenye thamani ya USD millioni 100;

viii. Kufanya tathmini ya Miradi mbali mbali inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo ikiwemo: Ujenzi wa Skuli tatu (Gamba, Kifundi na Mfenesini) unaotekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi mmoja na Ujenzi wa Nyumba za Madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani Pemba unaotekelezwa na Wizara ya Afya na Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Miundombinu ya Maji safi na salama unaotekelezwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini;

ix. Kushiriki katika Mikutano ya kikanda na kimataifa ya masuala ya Kodi pamoja na kujadili mkataba wa kuondoa utozaji kodi mara mbili (DTA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya CZECH, Qatar, Mauritius na majadiliano ya mkataba wa kifani (EAC MODEL TAX TREATY) na mkataba wa kuondoa utozwaji kodi mara mbili wa nchi za Afrika Mashariki (EAC MULTILATERAL DTA);

x. Kukamilisha Andiko la Dhana (Concept Note) kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji (Zanzibar Investment Bank) hatua inayoendelea ni majadiliano katika ngazi ya Serikali;

xi. Ofisi inaendelea kufanya mageuzi ya Bajeti ya Serikali yenye kuzingatia usawa wa kijinsia unaokwenda sambamba na dhana ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (5)

Zanzibar (ZADEP), Sera mbalimbali za sekta na utekelezaji wa Lengo Nambari 5 la Maendeleo Endelevu (SDGs). Katika mageuzi hayo, mipango na rasilimali fedha zitaelekezwa zaidi kupitia makundi mbalimbali yakiwemo wanawake, wanaume, wasichana, vijana, wazee, watu wenye mahitaji maalum, watoto na makundi mengineyo na mahusiano ya mahitaji yao katika jamii;

xii. Ofisi kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kutoka Shirika la Kuwahudumia Watoto Duniani (UNICEF) imefuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 katika sekta nne za kijamii ambazo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Katika zoezi hilo changamoto mbali mbali zimebainika ambazo zinachelewesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ikiwemo taratibu za manunuzi, kuchelewa kutoka kwa vifaa vya ujenzi bandarini na wazabuni kutoleta vifaa walivyokubaliana kwa wakati; na

xiii. Katika maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imejenga uwezo wa Wakurugenzi Mipango na Maafisa Mipango Waandamizi wa sekta, ili kuziwezesha Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti zinazoweza kuakisi matarajio ya wananchi.

***PF0102-Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma***

**29.** **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuwa na mfumo imara wa kusimamia mali za umma na uwekezaji wake. Hadi kufikia Machi 2024, programu hii imetumia **TZS 9.265 bilioni** sawa na asilimia **60** ya makadirio ya **TZS 15.318 bilioni** ya kipindi cha tathmini. Fedha hizo zimejumuisha **TZS 595.32 milioni** malipo ya mishahara, **TZS 1.386 bilioni** matumizi ya utekelezaji wa kazi za Ofisi, **TZS 5.652 bilioni** malipo ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali na **TZS 1.630 bilioni** fedha kwa ajili ya ruzuku kwa ajili ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA).

30. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kusimamia Mashirika (OTRMIS) kuhusiana na masuala ya kibajeti na fedha;

ii. Kuendelea na Ukamilishaji wa utayarishaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Umma (ZGAMIS);

iii. Kukamilika kwa Rasimu ya Muongozo wa Kusimamia Uondoshwaji wa Mali Chakavu katika Taasisi mbalimbali za Serikali; na

iv. Ofisi imekusanya jumla ya TZS 515.643 milioni kupitia kuuzwa kwa vifaa chakavu kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Wakala wa Barabara Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Mahkama Kuu Zanzibar na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

***PF0104– Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango***

31. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uendeshaji wa shughuli za sekta ya fedha. Hadi kufikia Machi 2024, programu hii imetumia jumla ya **TZS 16.044 bilioni** sawa na asilimia **92** ya makadirio ya **TZS 17.500 bilioni** na asilimia **9** ya makadirio ya **TZS 181.653 bilioni** kwa mwaka.Upungufu huo unatokana na kutokamilika kwa baadhi ya taratibu za utekelezaji wa miradi. Programu hii imejumuisha programu ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa OR-Fedha na Mipango hadi kufikia Machi 2024, imetumia jumla ya TZS 11.538 bilioni sawa na asilimia 217 ya makadirio ya TZS 5.313 bilioni. Ongezeko hili limetokana na kuanzishwa kwa Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi Zanzibar (ZIAAT), Idara ya Huduma za Sheria Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango pamoja na Idara ya Kusimamia Sera za Manunuzi. Fedha za kuendesha shughuli zao zimewekwa katika programu ndogo ya uendeshaji kwa kufanya uhaulishaji katika baadhi ya vifungu ndani ya Idara nyengine;

ii. Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti imetumia TZS 3.523 bilioni sawa na asilimia 35 ya makadirio ya TZS 10.162 bilioni ya kipindi cha tathmini. Fedha hizi zimejumuisha fedha za miradi ya maendeleo TZS 3.324 bilioni (ISP-DRM TZS 624 milioni na BIG-Z TZS 2.7 bilioni) na 196.561 milioni Fedha za uendeshaji wa Idara. Kuwepo na asilimia ndogo ya matumizi kwenye programu ndogo hii imetokana na fedha nyingi zilizopangwa kwenye miradi utelekelezaji wake ulikuwa mdogo shughuli nyingi zinatarajiwa  kutekelezwa katika kipindi cha April 2024; na

iii. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Pemba, imetumia jumla ya TZS 982.03 bilioni sawa na asilimia 49 ya makadirio ya TZS 2.024 bilioni ya kipindi cha tathmini.

**32. Mheshimiwa Spika,** Kiujumla Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Ofisi imefanya kikao cha kuimarisha ubora wa Takwimu za Kifedha (GFS) kwa kushirikiana na Washauri elekezi wa IMF, EAC na EAST AFRITAC, Kikao hicho kimewashirikisha wadau wa Takwimu za Fedha na kuweza kufanya mapitio ya takwimu za mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 kwa lengo la kuweka sawa mapungufu yaliyobainika pamoja na Kukuza ushirikiano katika uandaaji wa Takwimu za Kifedha pamoja na uandaaji wa ripoti ya pamoja ya takwimu baina ya Zanzibar na Tanzania Bara;

ii. Ofisi imefanya ufuatiliaji wa Miradi ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa kuitembelea na kufanya mahojiano na wahusika na imefanikiwa kutambua hatua mahsusi iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi pamoja na kubaini changamoto zinazo ikabili katika utekelezaji wake ikiwemo kubadilisha mawanda ya mradi na kutopatikana kwa hati miliki za maeneo ya miradi kwa wakati;

iii. Ofisi iliratibu uandaaji wa mpango wa matumizi ya muda wa kati (MTEF) kwa ajili ya matayarisho ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25;

iv. Ofisi iliandaa ripoti ya utekelezaji wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na Miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na ripoti ya miezi sita Julai–Disemba 2023/24 na kuiwasilisha katika Kamati ya Bajeti ya Baraza la wawakilishi;

v. Ufuatiliaji na usimamiaji wa matumizi wa mfumo wa ZANMALIPO katika Bandari ya Mkoani, Wete na Wesha ambapo utumiaji wa mfumo wa ZANMALIPO umeimarika kwa Taasisi zinazotoza tozo bandarini;

vi. Usimamiaji na uondoaji wa mali chakavu za Taasisi kumi na moja (11) zilizopo Pemba ambapo kiasi cha TZS 195.676 milioni zimekusanywa;

vii. Ofisi imefanya ziara ya ufuatiliaji wa taarifa za fedha na utekelezaji wa miradi kwa Asasi za Kiraia 31 kwa kipindi cha miezi sita (Julai – Disemba) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kutoka Wilaya zote nne za Pemba. Kati ya hizo Asasi 13 ndio zimepata fedha kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo na kutekeleza miradi mbali mbali ya kijamii ambapo kiasi cha TZS 1.517 bilioni zimepatikana na Asasi za Kiraia kwa kutekeleza miradi mbali mbali;

viii. Kupatiwa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 300 kati ya hao 100 walipatiwa mafunzo ya usalama kazini, 100 walipatiwa mafunzo ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na 100 walipatiwa mafunzo ya Sheria za Kazi na Maadili kwa Watumishi wa Umma;

ix. Jumla ya wafanyakazi 19 wanaoendelea mafunzo ya mda mrefu, kati yao 12 wanasoma ndani ya nchi na 7 wapo nje ya nchi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi;

x. Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za michezo ndani ya Wizara ambapo Wafanyakazi 35 wameshiriki katika michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Iringa na Mashindano ya ‘’Mapinduzi Cup” ya mwaka 2024. Aidha, wafanyakazi 50 walishiriki katika michezo ya kila mwaka ya Tamasha la Pasaka yaliyofanyika mkoani Dodoma; na

xi. Ofisi imeweza kufanikisha upatikanaji wa huduma bora za wafanyakazi ikiwemo mawasiliano, usafi, vitendea kazi na usafiri.

xii. Ofisi imeweza kufanya ununuzi wa gari 78 kati ya gari 229 zilizopangwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali, na jumla ya gari 151 zinatarajiwa kufika mwishoni mwa mwaka wa Fedha 2023/24.

**Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali)**

**33. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu F02 yanajumuisha programu kuu moja ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, programu hii imetumia jumla ya **TZS 214.955 bilioni** sawa na asilimia **106** ya makadirio ya **TZS 202.114 bilioni** ya kipindi cha tathmini na asilimia **83** ya makadirio ya **TZS 258.449 bilioni** kwa mwaka. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo: -

i. Malipo ya mishahara ya Viongozi Wakuu TZS 1.899 bilioni;

ii. Malipo ya marejesho ya Hati fungani na Riba ya Hati Fungani TZS 39.538 bilioni;

iii. Malipo ya marejesho ya Mikopo ya ndani TZS 30.559 bilioni;

iv. Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo kwa wastaafu 1,240 TZS 24.999 bilioni;

v. Malipo ya Pencheni Jamii TZS 13.840 bilioni;

vi. Malipo ya Pencheni kwa Wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya wastani wa 13,795 ya TZS 34.102 bilioni; na

vii. Matumizi mengineyo ya Serikali TZS 70.018 bilioni.

**Fungu F03 (Tume ya Mipango Zanzibar)**

**34. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu (F03) yanajumuisha programu kuu tatu (3) ndani yake kuna programu ndogo saba (7). Hadi Machi 2024, Fungu limetumia jumla ya TZS 3.517 bilioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya TZS 8.569 bilioni katika kipindi cha tathmini na asilimia 32 ya makadirio ya TZS 11.167 bilioni kwa mwaka. Mchanganuo wa matumizi kwa programu kuu ni kama ifuatavyo: -

***PF0301-Programu Kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi***

**35. Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mipango hiyo. Hadi Machi 2024, programu hii imetumia **TZS 1.762** bilioni sawa na asilimia **30** ya makadirio ya **TZS 5.811 bilioni** katika kipindi cha tathmini na asilimia **23** ya makadirio ya **TZS 7.759 bilioni** kwa mwaka. Programu hii inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini imetumia TZS 1.147 bilioni sawa na asilimia 36 ya makadirio ya TZS 3.185 bilioni ya kipindi cha tathmini;

ii. Programu ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu imetumia TZS 257.53 milioni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya TZS 637.538 milioni ya kipindi cha tathmini; na

iii. Programu ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo imetumia TZS 357.32 milioni sawa na asilimia 18 ya makadirio ya TZS 1.989 bilioni ya kipindi cha tathmini.

36. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi imetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya uhakiki wa Programu za maendeleo Unguja na Pemba zikiwemo Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria katika eneo la Ras-Mkumbuu Pemba, Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu, Programu ya Uimarishaji Miundombinu ya Elimu, Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi na Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia;

ii. Miradi mbali mbali imefanyiwa uhakiki ikiwemo Ujenzi wa Mahkama za Mikoa; mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Mawasiliano; mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar; mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar; Ujenzi wa Uwanja wa Amani; mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi; mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani; Ujenzi wa Masoko ya wafanyabiashara Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini na mradi wa Uimarishaji wa Shughuli za Taasisi za Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar;

iii. Tume ya Mipango Zanzibar kwa kushirikiana na Tume ya Mipango Tanzania, inaratibu zoezi la kuandaa Dira ya Taifa 2050. Kwa upande wa Zanzibar kulifanyika semina elekezi ya uhamasishaji wananchi kushiriki katika zoezi la ukusanyaji maoni kwa watendaji wa Serikali 255 katika ngazi za Mikoa yote ya Zanzibar. Pia kulifanyika zoezi la majaribio ya utoaji wa maoni kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao ulikuwa ni miongoni mwa Mikoa iliyochaguliwa kati ya Mikoa mitano (5) ya Zanzibar;

iv. Kushiriki kikao cha mashirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Misaada la Japan (JICA) na Uturuki kujadili programu/miradi itakayofadhiliwa na nchi hizo. Pamoja na kushiriki katika kikao cha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika bajeti za Wizara na Taasisi za Serikali (Gender

Responsive Budget) kwa lengo la kuingiza masuala ya kijinsia katika shughuli za maendeleo ili isaidie kuleta maendeleo yenye kuzingatia haki na usawa wa kiuchumi;

v. Tume kwa kushirikiana na TASAF imeandaa andiko la utafiti wa hali ya umasikini Tanzania. Kwa upande wa Zanzibar utafiti huu utajumuisha maeneo yaliyoainishwa kuwa yana umasikini zaidi katika ripoti ya tathmini ya Mapato na Matumizi ya Kaya ya mwaka 2019/20 (Household Budget Survey). Utafiti huu unatarajiwa kufanyika katika Wilaya ya Kaskazini "B" na Kusini Unguja na Wilaya ya Micheweni kwa Pemba;

vi. Kuimarisha mfumo wa Shehia Regista kwa kuunganishwa na mfumo wa Geographical Information System (GIS) kwa kuingiza taarifa za majengo. Kwa kuanzia Shehia ya Sokoni Mwanakwerekwe imeingizwa taarifa zake ambapo majengo 798 yamerikodi kwa kutumia program elekezi ya 'Margin Map'. Aidha, ramani za mipaka ya Shehia na Zoni kwa kutumia programu wezeshi ya Q–GIS zimetayarishwa kwa Shehia zote za Wilaya ya Mjini ili kurahisisha zoezi la kuingizwa kwa taarifa za majengo na idadi ya Kaya;

vii. Kufanya Mapitio na mafunzo ya mfumo wa kidigitali wa Mipango ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Miradi na Programu za Maendeleo. Jumla ya maafisa ufuatiliaji na tathmini na Maafisa mipango 50 sawa na asilimia 80 ya wafanyakazi waliopangwa kupewa mafunzo walishiriki mafunzo hayo kutoka Wizara zote; na

viii. Kufanya mapitio ya Mpango wa Maendeleo Zanzibar (ZADEP 2021-26). Kazi hii inaendelea na kwa sasa ipo katika hatua ya kukamilisha muongozo ili kuanza kazi ya kukusanya taarifa. Viashiria vya matokeo tayari vishawasilishwa sekta ili kupata taarifa za viashiria hivyo.

***PF0302-Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti***

37. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia sera za kiuchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa vya Tafiti zitakazosaidia ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu. Hadi Machi 2024, programu imetumia jumla ya **TZS 503.80 milioni** sawa na asilimia **42** ya makadirio ya **TZS 1.193 bilioni** katika kipindi cha tathmini na asilimia **37** ya makadirio ya **TZS 1.370 bilioni** kwa mwaka. Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni:-

   i. Programu ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi, hadi Machi 2024, imetumia jumla ya TZS 248.58 milioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya TZS 320.661 milioni ya kipindi cha tathmini; na

   ii. Programu ndogo ya Utafiti imetumia jumla ya TZS 255.23 milioni sawa na asilimia 29 ya makadirio ya TZS 872.929 milioni ya kipindi cha tathmini.

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti imetekeleza shughuli zifuatazo: -

   i. Kuwasilisha ripoti tisa (9) za kujadili hali ya mfumko wa bei katika Kamati ya Ukomo wa matumizi ya kila mwezi (Ceiling Committee) na ripoti tatu (3) za Mwenendo wa Hali ya Uchumi kwa kila robo mwaka kwa kuwashirikisha wahusika kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali zikiwemo Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania;

   ii. Kuratibu tafiti tatu (3) za Kimkakati ikiwemo Utafiti wa Kuchunguza Athari za Kiuchumi na Kijamii Zinazotokana na Ajali za Barabarani kwa Zanzibar ili kubaini vyanzo na kupendekeza njia zitakazotumika kupunguza athari hizo, kukamilika kwa Ripoti ya Utafiti wa Uchunguzi wa Saratani ya Shingo ya Uzazi kwa Kinamama na kutayarisha kwa andiko la awali kwa ajili ya Utafiti wa Zao la Karafuu;

iii. Ofisi kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Chuo kikuu cha Taifa (SUZA) imepitia na kujadili Muongozo wa Usimamizi wa Tafiti na Fedha za Tafiti (Research, Innovation and Grant Management Guidelines). Aidha, kikao kimoja (1) cha ushauri cha kitaalamu (Consultative Stakeholders Meeting) kimefanyika ikijumisha maafisa 32 kutoka Serikalini kwa Unguja na rasimu za muhtasari wa Sera tatu (3) zimeandikwa na kuwasilishwa ili kupata maoni yatakayosaidia kuimarisha na kutangaza matokeo ya tafiti hizo; na

iv. Kituo mama cha ubunifu cha Maruhubi (iBUA - Innovation Hub) kimeanzishwa ambapo jumla ya wakuu wa vituo vya ubunifu 30 wamepatiwa mafunzo ya kuendesha vituo vya ubunifu Zanzibar. Kituo hiki kitaongeza kazi za ubunifu na kuchangia ongezeko la ajira kwa vijana.

***PF0303-Programu Kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango***

39. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Hadi Machi 2024, programu imetumia jumla ya **TZS 1.251 bilioni** sawa na asilimia **80** ya makadirio ya **TZS 1.563 bilioni** katika kipindi cha tathmini na asilimia **61** ya makadirio ya **TZS 2.036 bilioni** kwa mwaka. Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango imetumia jumla ya TZS 973.10 milioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya TZS 1.245 bilioni ya kipindi cha tathmini; na

ii. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Tume ya Mipango Pemba imetumia TZS 278.02 milioni sawa na asilimia 87 ya makadirio ya TZS 426.11 milioni ya kipindi cha tathmini.

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mafunzo mtambuka yametolewa kwa wafanyakazi wa Tume ya Mipango katika kufahamu na kujilinda na athari zitokanazo na afya ya akili na msongo wa mawazo katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao;

ii. Kuimarisha utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Umma kwa wafanyakazi wa Tume ya Mipango kwa Unguja na Pemba ambapo wafanyakazi 101 walishiriki na waliweza kutoa maoni ili kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi pamoja na kujengewa uelewa juu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango wa kipindi cha 2023-2025;

iii. Mafunzo yametolewa ya Muda Mrefu kwa wafanyakazi 12 na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 45 katika fani zinazohusiana na kada zao ikiwemo mipango, Sheria, uchumi na uhusiano ili kuimarisha utendaji; na

iv. Kuratibu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Tume ya Mipango zinazofanyika kwa upande wa Pemba kwa kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayoendelea kutekelezwa kwa upande wa Pemba na kushiriki vikao kazi vinne (4) kwa Maafisa Mipango na Maafisa Wadhamini Pemba na Vikao vya Uongozi Unguja.

**Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)**

41. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Fungu F04 limetumia jumla ya TZS 3.35 bilioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya kutumia TZS 8.27 bilioni ya mwaka. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu Kuu zifuatazo:-

***PF0401-Programu Kuu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii***

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuongeza ubora na wingi wa takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Programu

hii kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, imetumia **TZS 2.4 bilioni** sawa na asilimia **40** ya makadirio ya kutumia **TZS 5.97 bilioni** kwa mwaka.Programu hii kuu imejumuisha programu ndogo mbili:-

i. Programu ndogo ya Ukusanyaji, Uchambuzi na Uwasilishaji wa Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii. Programu hii imetumia TZS 1.72 bilioni sawa na asilimia 36 ya makadirio ya kutumia TZS 4.76 bilioni kwa mwaka; na

ii. Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Kitakwimu katika Mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar. Programu hii imetumia TZS 669.27 milioni sawa na asilimia 55 ya makadirio ya kutumia TZS 1.22 bilioni kwa mwaka.

**43. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imetumia fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ofisi imekusanya, imechakata, imekamilisha na kutoa ripoti mbalimbali za kitakwimu za kila mwezi na robo mwaka na kusambazwa kwa wadau kwa njia ya Tovuti, machapisho na Vyombo vya Habari; Ripoti 58 zimetolewa zikijumuisha ripoti 43 za kila mwezi na ripoti 15 za robo mwaka. Aidha, Ripoti hizo zinajumuisha; Takwimu za Faharisi ya Bei ya Mlaji, Takwimu za wageni wanaoingia Nchini, Takwimu za Pato la Taifa, Takwimu za matukio ya Ajali na Makosa ya Barabarani, Takwimu za Usafiri, pamoja na Takwimu za Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto; na

ii. Katika kusimamia shughuli za Tafiti, Ofisi imetoa ushauri wa kitaalamu kwenye Taasisi zinazoendesha tafiti na kutoa vibali vya kuendesha tafiti hizo ambapo hadi kufikia Machi, jumla ya vibali 577 vimetolewa kati ya hivyo, vibali 481 vilitolewa kwa wanafunzi, vibali 37 vilitolewa kwa Taasisi, vibali 55 vilitolewa kwa Wageni na vibali 4 vimetolewa kwa watu binafsi (wazawa).

***PF0402-Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Utawala na Uendeshaji hadi Machi 2024 Programu hii imetumia jumla ya **TZS 963.56 milioni** sawa asilimia **42** ya makadirio ya kutumia **TZS 2.29 bilioni** kwa mwaka. Programu kuu hii imejumuisha programu ndogo mbili nazo ni:-

   i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja. Programu hii imetumia TZS 703.53 milioni sawa na asilimia 42 ya makadirio ya kutumia TZS 1.66 bilioni kwa mwaka; na

   ii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Takwimu Pemba, imetumia TZS 260.03 milioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya kutumia TZS 631.52 milioni kwa mwaka.

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imetumia fedha kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

   i. Kusimamia stahiki za watumishi ambapo kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024, watumishi 23, wamepatiwa likizo kati ya hao watumishi 16 wamepatiwa posho la likizo;

   ii. Katika Kuimarisha utendaji kazi, Ofisi imeratibu Mpango wa Rasilimali watu wa miaka mitano (5) kwa kuingiza taarifa za kiutumishi za watumishi wote wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika Mfumo wa kielektroniki; na

   iii. Matumizi ya uendeshaji wa Ofisi yamefanyika ikiwemo ununuzi wa vifaa mbali mbali vya uendeshaji vikiwemo vifaa vya kuandikia, mafuta na samani mbali mbali za Ofisi. Aidha, huduma ya maji, usafi, umeme na mawasiliano zimetolewa.

**Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)**

46. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali hadi Machi 2024, imetumia jumla ya TZS 8.81 bilioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya kutumia **TZS 10.8 bilioni** kwa kipindi cha tathmini na

asilimia 79 ya makadirio ya kutumia **TZS 11.14 bilioni** kwa mwaka na fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu kuu zifuatazo:-

***PF0501 – Programu Kuu ya Usimamizi wa Hazina***

**47. Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2024, program hii imetumia jumla ya TZS 175.42 milioni sawa na asilimia 34 ya makadirio ya kutumia TZS 518.4 milioni kwa kipindi cha tathmini na asilimia 26 ya makadirio ya kutumia TZS 664.3 milioni kwa mwaka. Programu kuu hii imejumuisha programu ndogo nne nazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali Yasiyokuwa ya Kodi. Programu hii hadi Machi imetumia TZS 23.57 milioni sawa na asilimia 28 ya makadirio ya kutumia TZS 84.15 milioni kwa kipindi cha tathmini;

ii. Programu Ndogo ya Kusimamia ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali. Programu hii hadi Machi imetumia jumla ya TZS 14.19 milioni sawa na asilimia 31 ya makadirio ya kutumia TZS 46.44 milioni kwa kipindi cha tathmini;

iii. Programu ndogo ya Usimamizi wa Matumizi ya Serikali. Programu hii hadi Machi imetumia jumla ya TZS 59.61 milioni sawa na asilimia 50 ya makadirio ya kutumia TZS 118.66 milioni kwa kipindi cha tathmini; na

iv. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Deni la Taifa. Programu hii hadi Machi imetumia jumla ya TZS 78.05 milioni sawa na asilimia 29 ya makadirio ya kutumia TZS 269.15 milioni kwa kipindi cha tathmini.

**48. Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii imetumia fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kufanya ufuatiliaji wa mapato katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa Unguja ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kujua matatizo yanayowakabili ambayo yanasababisha kutofikia malengo yaliowekwa;

ii. Kupitia hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali ili kuhakikisha zinafuata miongozo ya ufungaji hesabu iliopo;

iii. Kusimamia na kuwaongoza Watumiaji wa Mfumo katika kazi zao za kila siku, kutoa haki za utumiaji wa Mfumo kwa Watumiaji "user access rights", kuingiza watoa huduma katika Mfumo "Vendors", kutoa msaada wa kitalaamu kwa watumiaji wa mfumo pamoja na kutatua changamoto zilizojitokeza na kuendelea na kufanya majaribio katika "modules" mbalimbali zilizomo katika mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS) kwa ajili ya kutambua changamoto na kuzitafutia ufumbuzi wa mapema; na

iv. Kufanya uhakiki wa wastaafu 12,150 kati ya wastaafu 14,324 Unguja na Pemba waliotumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

***PF0502 – Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali***

49. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2024, program hii imetumia jumla ya **TZS 8.63 bilioni** sawa na asilimia **84** ya makadirio ya kutumia **TZS 10.28 bilioni** kwa kipindi cha tathmini na asilimia **82** ya makadirio ya **TZS 10.48 bilioni** ya mwaka. Programu kuu hii imejumuisha program ndogo zifuatazo:-

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja. Programu hii hadi Machi imetumia jumla ya TZS 6.66 bilioni; na

ii. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Pemba. Programu hii hadi Machi imetumia jumla ya TZS 1.97 bilioni.

50. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imetumia fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kujenga uwezo wa wahasibu kwa lengo la kuimarisha utendaji ambapo wahasibu 5 walishiriki katika Mkutano wa Mwaka wa Wahasibu na Wakaguzi uliofanyika Arusha, wahasibu 8 wameshiriki mafunzo ya kuongeza masaa ya kitaalamu (CPD

– Hours), kuwalipia ada ya mwaka wafanyakazi 8 wenye CPA pamoja na kugharamia mafunzo ya CPA na IPSAS;

ii. Kuratibu ujio wa wataalamu kutoa IMF AFRITAC EAST ambao walikuja kwa lengo la kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhama kutoka katika utaratibu wa kufunga hesabu kwa kutumia "Cash Basis" na kuhamia katika "Accrual Basis";na

iii. Matumizi mengineyo ya uendeshaji wa Ofisi ya kusimamia fedha za umma na kuimarisha shughuli za uhasibu serikalini kwa upande wa Pemba.

**Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali)**

51. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali hadi Machi 2024, imetumia jumla **TZS 4.53 bilioni** sawa na asilimia **114** ya makadirio ya **TZS 3.97 bilioni** kwa kipindi cha tathmini na asilimia **87** ya makadirio ya kutumia **TZS 5.19 bilioni** kwa mwaka. Ongezeko hilo la matumizi linatokana na kuongezeka mishahara ambapo makadirio ya awali yalikuwa madogo. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu Kuu zifuatazo: -

***PF0601-Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani (ISP-DRM)***

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii hadi Machi 2024, imetumia **TZS 33.1 milioni** sawa na asilimia **18** ya makadirio ya kutumia **TZS 187.1 milioni** kwa kipindi cha tathmini na asilimia **16** ya makadirio ya kutumia **TZS 210.6 milioni** kwa mwaka. Upungufu wa matumizi umetokana na baadhi shughuli kutofanyika kwa uhaba wa Fedha za matumizi mengineyo. Programu kuu hii imejumuisha programu ndogo zifuatazo: -

i. Programu Ndogo ya Uchunguzi wa Ubadhirifu na Vihatarishi. Programu hii hadi Machi imetumia jumla ya TZS 25.26 milioni; na
ii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uthibitisho wa Ubora. Programu hii hadi Machi imetumia TZS 7.85 milioni.

**53. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imetumia fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya Kaguzi Maalum ambapo zilihusisha Wizara ya Afya, Kamisheni ya Utalii, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika mradi wa HEET, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) pamoja na Ujenzi wa vyoo maeneo ya Chunga na Kihinani katika Baraza la Manispaa Magharibi "A". Ukaguzi huo umefanyika kwa lengo la kuongeza udhibiti wa ndani wa Fedha;

ii. Kutengeneza Muongozo wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi ambao utaenda kutumika katika Taasisi zote za Serikali. Muongozo huo umefikia hatua ya kupata maoni ya wadau ambapo jumla ya vikao vitatu vimefanyika kwa ajili ya kuchukua maoni ya wadau Unguja na Pemba;na

iii. Kufanya uhakiki wa ubora kwa vitengo 16 vya ukaguzi wa ndani zikiwemo Taasisi 11 Unguja na Taasisi tano (5) kwa upande wa Pemba. Uhakiki huu ulifanyika kwa kuangalia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 na Kanuni yake ya mwaka 2021. Uhakiki pia uliangalia utekelezaji wa muongozo wa ukaguzi wa ndani pamoja na Muongozo wa Ukaguzi wa Kimataifa unaosimamia viwango vya ukaguzi wa ndani (IPPF).

### *PF0602- Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji*

**54. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Programu hii imetumia **TZS 4.49 bilioni** sawa na asilimia **119** ya makadirio ya kutumia **TZS 3.8 bilioni** kwa kipindi cha tathmini na asilimia **90** ya makadirio ya fedha ya **TZS 4.98 bilioni** kwa mwaka. Programu hii imejumuisha programu ndogo zikiwemo:-

i. Program Ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Mafunzo na Utafiti. Hadi Machi, imetumia jumla ya TZS 3.7 bilioni sawa na asilimia 117 ya makadirio ya kutumia TZS 3.16 bilioni kwa kipindi cha tathmini;na

ii. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba hadi Machi imetumia jumla ya TZS 782.4 milioni sawa na asilimia 126 ya makadirio ya kutumia TZS 620 milioni kwa kipindi cha tathmini.

**55. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imetumia fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wakaguzi wa ndani katika fani za CIA ambapo jumla ya wakaguzi wa ndani 11 wanaendelea na mafunzo hayo;

ii. Mafunzo ya Mbinu za Kukagua Utekelezaji (Performance Audit Techniques) yametolewa kwa Wakaguzi wakuu wa ndani 45 wa Unguja na Pemba juu ya masuala ya manunuzi, usimamizi wa mikataba pamoja na usimamizi wa miradi kwa lengo la kuboresha ufanisi katika kazi za ukaguzi;

iii. Kuandaa taarifa jumuishi ya ukaguzi wa ndani za Wizara na Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

iv. Kuandaa rasimu ya Sheria ya Ukaguzi wa Ndani ili kutoa muongozo wa ukaguzi wa ndani na uendeshaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani.

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA OFISI YA RAIS -FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2023/2024

### Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu ina lengo la kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi ulipangiwa TZS 1.72 bilioni. Hadi kufikia Machi 2024, Programu imetumia **TZS 624.0 milioni** sawa na asilimia **36** ya makadirio ya mwaka 2023/24. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuandaa Rasimu ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato Yatokanayo na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kutengeza GFS codes; ambapo imewasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba kwa kutoa maoni;

ii. Kuandaa Rasimu ya Sera ya Madini na mkakati wake, ambapo hatua iliyofikiwa ni kuiwasilisha kwa wadau Unguja na Pemba kupata maoni.

**Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)**

**57. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar ina lengo la kuimarisha miundombinu, haiba ya Zanzibar na kukuza Maendeleo ya kiuchumi katika utoaji wa huduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii ilikadiriwa kutumia **TZS 22.8 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi Machi 2024, jumla ya **TZS 2.7 bilioni** sawa na asilimia **12** ya fedha iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/24 zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ofisi imeajiri Mshauri Elekezi (Dar Al-handasah) kwa ajili ya kazi ya mapitio na upembuzi yakinifu, usarifu wa michoro, kuandaa nyaraka za zabuni na kusimamia ujenzi wa mradi wa kuendeleza eneo la Michenzani na Mradi Salama wa Watembea kwa Miguu Mji Mkongwe. Mshauri Elekezi ameanza kazi Machi, 2024;

ii. Mikataba mitatu (3) imesainiwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi kwa mabaraza ya miji na Manispaa za Unguja na Pemba;

iii. Ripoti ya Tathmini ya Fidia imewasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ithibati ya ulipaji wa fidia kwa waathirika wa Mradi wa Kuimarisha Miji Unguja (AUP-Unguja) ikiwemo eneo la **Ziwa Maboga.**

iv. Imeajiri Mshauri Elekezi wa kampuni ya ARS Progetti SPA kwa ajili ya kazi yakufanya upembuzi yakinifu, usarifu wa michoro, kuandaa nyaraka za zabuni na kusimamia ujenzi wa Mradi wa

Kuimarisha Maeneo ya Utalii katika vijiji vya Nungwi, Chwaka na Makunduchi (IPLAD) na tayari Mshauri Elekezi amewasilisha Ripoti ya Awali (inception report);

v. Ofisi imesaini Mkataba na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi ya kufanya upembuzi yanikifu, usarifu wa michoro, kuandaa, nyaraka za zabuni na kusimamia ujenzi wa mradi wa Kuimarisha maeneo ya miji ya Pemba (AUP-Pemba), kazi imeanza na hatua inayofuata ni kuwasilisha ripoti ya awali (inception report) ya utekelezaji wa mradi; na

vi. Imekamilisha hatua za awali za kuondosha taka na tope katika eneo la **Bwawa la Mwantenga** ili kupunguza athari za mafuriko katika eneo hilo.

**Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**

**58. Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuimarisha utendaji kazi kwa kupata vitendea kazi, mifumo ya kielektroniki na ujuzi kwa wafanyakazi na hatimaye kuimarisha usimamizi mzuri wa Fedha za Umma. Programu hii inatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu ilipangiwa jumla ya **TZS 3.89 bilioni** Hata hivyo, kwa kipindi cha Julai - Machi fedha hizo hazijapatikana na kukosa kutekeleza kwa kazi za Programu hii.

**Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali**

**59. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi ili kuimarisha ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa wananchi. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 programu imepangiwa **TZS 74.12 bilioni,** Fedha hizo zimejumuisha **TZS 55.078 bilioni** za Ujenzi wa Mji wa Serikali na **TZS 19.044 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi za Serikali.

**60. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Ujenzi wa Mji wa Serikali hadi sasa hakuna fedha iliyotumika. Hata hivyo, mazungumzo ya awali yamefanyika kwa waathirika sita (6) wanaoishi katika eneo

husika la Kisakasaka kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na kulipwa fidia. Aidha mazungumzo yanaendelea na mbia aliejitokeza kutaka kushirikiana na serikali katika ujenzi huo.

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Ujenzi na ukarabati wa ofisi za Serikali hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TZS 5.65 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **30** ya makadirio ya mwaka. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Ujenzi wa jengo Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC);

ii. Kuendelea na Ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA);

iii. Ujenzi wa Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar; na

iv. Kuboresha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

**Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar**

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 2.50 bilioni**. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya **TZS 911.91 milioni** zilitumika sawa na asilimia **36** ya fedha iliyopangwa kwa mwaka kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kupima viwanja 1,575 (Unguja 814 na Pemba 761) katika maeneo ya Mbweni, Gombani, Konde na Utaani na kutolewa hati 570 za matumizi ya Ardhi;

ii. Ununuzi wa Makabati ya kielektroniki ya kuhifadhia nyaraka za Ardhi katika Jengo la Masjala ya Ardhi Mwanakwerekwe, pamoja na kupatiwa mafunzo ya matumizi yake;

iii. Kufuatilia shughuli za programu ya Urasimishaji wa Ardhi na Biashara Zanzibar kwa kuangalia wafanyabiashara waliopatiwa

mafunzo ya uendeshaji wa biashara katika Wilaya ya Wete Pemba pamoja na kutembelea kituo cha urasimishaji wa Biashara Chake chake Pemba na Wilaya ya Kaskazini "A" kwa Unguja;

iv. Kuendelea na Ujenzi wa Jengo la Masjala ya Ardhi Makunduchi kwa sasa lipo katika hatua za kukamilisha uwekaji wa milango, madirisha pamoja na mifumo ya umeme; na

v. Kuwapatia mafunzo Wafanyabiashara 200 katika Wilaya ya Chake Chake na Kaskazini A kati ya hao, wafanyabiashara 153 wamesajili Biashara zao (Chake Chake 82 na 71 Kaskazini "A").

**Mradi wa Usimamizi wa Kufanya Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi ya Maendeleo**

63. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kufanya uratibu na usimamizi wa uandaaji wa upembuzi yakinifu na Mapitio ya Sekta za kijamii na kiuchumi. Mradi ulikadiriwa kutumia TZS 1.50 bilioni, kutoka Serikalini hadi kufika Machi 2024 hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi huo.

**Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa**

64. **Mheshimiwa Spika,** Mradi una lengo la kuimarisha Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha **TZS 2.0 bilioni** kutoka Serikalini hadi kufikia machi 2024 hakuna fedha iliotumika katika mradi.

**Programu ya Uimarishaji wa Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II)**

65. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar ikiwemo kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji

na utoaji wa takwimu za kawaida kwa wakati, kuweka mazingira mazuri ya kuratibu upatikanaji wa viashiria na takwimu za Kiuchumi na Kijamii kupitia takwimu za kawaida, Sensa na tafiti. Katika kipindi cha Utekelezaji Programu imelenga kuwezesha Uzalishaji na Usimamizi wa Takwimu, Uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, Maendeleo ya Rasilimali Watu pamoja na Mfumo wa Kisheria. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imekadiriwa kutumia jumla **TZS 4.4 bilioni** hadi Machi 2024, imetumia jumla ya **TZS 1.313 billioni** sawa na asilimia 30 ya fedha zilizopangwa kwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

***Utafiti wa kilimo***

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa Kilimo ulifanyika kwa Tanzania nzima, kwa upande wa Zanzibar jumla ya maeneo ya kuhesabia watu yapatayo 118 yalipitiwa. Utafiti huo umelenga kuimarisha upatikanaji wa takwimu za kilimo kuwa zenye uwiano unaofuata miongozo ya kimataifa pamoja na kutoa viashiria vya muda mfupi na muda mrefu. Aidha Ofisi inaendelea kufanya tafiti nyengine ikiwemo, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya kaya (HBS), Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi mwaka 2024 (ILFS) na Ukusanyaji wa Taarifa za Utafiti wa Ajira na Mapato kwa mwaka 2022/23.

***Sensa ya Shughuli za Kiuchumi na Kijamii (CRE)***

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Sensa hii ina lengo la kuzitambua Taasisi pamoja na shughuli zinazofanywa na Taasisi hizo ili iwe “Frame” kwa ajili ya Tafiti mbali mbali zinazohusiana na Taasisi hizo. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 kazi inayoendelea ni usafishaji wa taarifa (data cleaning) na uandishi wa ripoti baada ya kukamilika kwa kazi ya ukusanyaji wa taarifa ambapo jumla ya taasisi 40,175 zimefikiwa na sensa hiyo.

## E. UTEKELEZAJI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS -FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2023/2024

### Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

68. **Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai - Machi 2024, ZRA ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 479.178 bilioni** hadi kufikia Machi 2024, ZRA imekusanya jumla ya **TZS 559.484 bilioni** ambazo ni sawa na asilimia **117** katika kipindi cha tathmini. Kwa kulinganisha na makusanyo halisi ya kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023 ya **TZS 449.283 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia **25** ya makadirio **TZS 460.499 bilioni.** Ongezeko hili limetokana na kuimarika kwa usimamizi wa sheria za kodi, kuendelea vizuri kwa kasi ya ukuaji wa uchumi na ongezeko la wageni walioingia nchini.

69. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zifuatazo pia zimechangia ukusanyaji wa mapato ambazo ni:-

i. Matumizi ya mifumo, usimamizi wa matumizi ya mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki (VFMS), pamoja na uimara na upatikanaji kwa wakati wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ndani ya Mamlaka;

ii. Kusajili walipa kodi wapya, katika kuhakikisha kwamba kila anayelazimika kusajiliwa kulipakodi kwa mujibu wa sheria anasajiliwa ili kutanua wigo wa kodi, Jumla ya walipakodi wapya 4,519 wamesajiliwa. Kati ya hao ni Kodi ya Ongezeko la Thamani 422, Ushuru wa Hoteli 107, Ushuru wa Mikahawa 52, Ushuru wa Watembeza Wageni 79, Ushuru wa Stempu 1,592, Ushuru wa Bidhaa 3, Kodi ya Ardhi 80, Kodi ya Jengo 2,158, Ada ya Uwanja wa Ndege 1, Ada ya Bandari 3, na Kodi ya zuwio 22;

iii. Uweledi na uadilifu kwa wafanyakazi, kuendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Mamlaka kuweza kutoa huduma bora zaidi kwa walipakodi pamoja na Uwajibikaji wa Hiari wa walipa kodi ;

iv. Kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara;

v. Kuimarika kwa ushirikiano na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii, Ofisi za Uhamiaji pamoja na uwepo wa mahusiano mazuri na walipakodi; na

vi. Uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane.

70. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2024, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilikadiria kutumia jumla ya **TZS 18.650 billioni** kwa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo. Matumizi halisi ni **TZS 17.672 billioni** sawa na asilimia **95** ya makadirio. Kati ya fedha hizo **TZS 3.922 billioni** zilitumika kwa kazi za Maendeleo na **TZS 13.750 billioni** zilitumika kwa kazi za kawaida.

**Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

71. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar imefanikiwa kukusanya kiasi cha **TZS 384.366 bilion**i ya makadirio ya kukusanya **TZS 383.978 bilioni** sawa na asilimia **100** ya lengo la kipindi hicho. Mafanikio haya yametokana na:-

i. Uboreshaji wa mifumo ya Forodha na kodi za ndani (Enhancement TANCIS na Up Graded E-Filing System), ambapo mifumo hii humrahisisshia mfanyabiashara kujikadiria kodi mwenyewe na kutengeneza control Number ya malipo;

ii. Ufunguzi wa vituo viwili (Tax Centre) vilivyopo Kiwengwa na Paje;

iii. Ununuzi wa Scanner mpya ya kisasa kwa lengo la kuzuia na kulinda bidhaa zitakazoleta madhara zinazoingia Nchini kwa

matumizi ya Majumbani, Kusaidia uwezeshaji wa biashara (Trade Facilitation). katika kipindi cha Julai 2023 hadi March 2024 Ofisi imefanikiwa kuchunguza (scan) makasha 1,852 na Kurahisisha utoaji wa mizigo bandarini kwa kupunguza muda wa ukaguzi; na

iv. Kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi kutoka 134 hadi 218.

**Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)**

72. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ZPPDA, imekadiriwa kukusanya **TZS 750 milioni** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato ikiwemo usajili wa watoa huduma, ada ya mafunzo ya mpango wa manunuzi, ada ya nyaraka za zabuni na matangazo ya zabuni. Hadi Machi 2024, Mamlaka imekusanya **TZS 363 milioni** sawa na asilimia **48** ya makadirio.

73. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, hadi Machi 2024, Mamlaka imetumia jumla ya **TZS 1.630 bilioni** sawa na asilimia **62** ya kupokea ruzuku ya **TZS 2.617 bilioni** kwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kukagua Taasisi nunuzi 30 Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha usimamiaji na utumiaji wa Sheria unatekelezwa ipasavyo;

ii. Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya mfumo wa ununuzi wa mtandao (e-Proz) kwa Bodi ya Zabuni na watendaji wa ununuzi kwa Taasisi nunuzi 45 kwa awamu ya kwanza na Taasisi 55 kwa awamu ya pili na watoa huduma 321 kwa upande wa Unguja na Taasisi 54 na Watoa Huduma 221 kwa upande wa Pemba;

iii. Mamlaka imesajili watoa huduma 1,822 kwa kupitia mfumo wa ununuzi wa mtandao (e-Proz);

iv. Kutayarisha nyaraka sanifu (1) ya huduma ya Mshauri elekezi (standard bidding document for individual consultancy);

v. Kufanya Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya Mwaka 2016; na

vi. Kufanya vikao vya kujadili changamoto za ununuzi na kutoa mapendekezo na ushauri wa kimanunuzi kwa Taasisi nunuzi na Idara Maalum za SMZ.

**Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)**

**74. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulikadiria kupata mapato ya **TZS 174.34 bilioni** kutoka katika vyanzo vikuu viwili, ambavyo ni **TZS 110.25 bilioni** ni michango ya wanachama na **TZS 64.09 bilioni** mapato ya uwekezaji. Mchanganuo wa mapato hayo kupitia vyanzo hivyo kama ifuatavyo:-

**75. Mheshimiwa Spika,** Michango ya wanachama hadi kufikia Machi 2024, Mfuko ulikusanya **TZS 111.45 bilioni** sawa na asilimia **101** ya makadirio ya kukusanya **TZS 110.25 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia **15** ya makusanyo **TZS 97.28 bilioni** ukilinganisha na kipindi kama hicho 2022/2023.

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024 Mfuko umepata mapato ya uwekezaji **TZS 66.15 bilioni** dhidi ya makadirio ya kupata **TZS 64.09 bilioni** sawa na asilimia **103,** ukilinganisha na kipindi kama hiki mwaka uliopita kulipatikana **TZS 46.19 bilioni** ikiwa ni ongezeko la asilimia **43.**

**77. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024 Mfuko ulipanga kutumia jumla ya **TZS 267.5 bilioni** hadi Machi 2024, Jumla ya **TZS 245.36 bilion**i zilitumika sawa na asilimia **92.** Mchanganuo wa Matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Malipo ya mafao ya wanachama TZS 56.09 bilioni;

ii. Matumizi kwaajili ya Uwekezaji TZS 180.95 bilioni;

iii. Usimamizi wa miradi TZS 1.15 bilioni; na

iv. Gharama za uendeshaji TZS 7.17 bilioni.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mfuko ulitekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Mfuko umesajili waajiri 237 sawa na asilimia 98 ya makisio ya kuwasajili waajiri 243. Hadi sasa Mfuko umekuwa na Waajiri waliosajiliwa kufikia 3,029;

ii. Mfuko umesajili waajiriwa 8,827 sawa na asilimia 63 ya makisio ya kuwasajili waajiriwa 13,988. Wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi Machi 2024, wamefikia 128,995 kwa Mfuko wa lazima;

iii. Waajiri 1,085 walitarajiwa kufanyiwa ukaguzi. Waajiri 1,765 wamekaguliwa, kati ya hao waajiri 750 walikaguliwa kwa ufuatiliaji (Follow-up), waajiri 702 walikaguliwa kwa ukaguzi wa kawaida (Routine) na waajiri 313 walikaguliwa katika zoezi la ukaguzi la waajiri wapya (Survey Inspection);

iv. Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar unaendelea kukusanya michango ya asilimia moja (1%) kutoka kwa waajiri kuhusiana na Fao la kuumia kazini;

v. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Majengo 14 yanaendelea kujengwa na utekelezaji umefikia asilimia 85 na mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi;

vi. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa maegesho ya gari Malindi, kwa sasa mradi huo unaendelea na ujenzi na utekelezaji umefikia asilimia 75. Mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi;

vii. Kwa upande wa mradi wa kituo cha mabasi Kijangwani, Mfuko ulitumia Utaratibu wa Usanifu na ujenzi na kwa sasa Mkandarasi wa mradi huo anaendelea na ujenzi na utekelezaji umefikia asilimia 60. Mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi;

viii. Ujenzi wa mradi wa Michezo na Biashara Mbweni; mradi unaendelea na hatua iliyofikia uwekaji "interlock" katika eneo la kuegeshea gari, sehemu ya "swimming pool" inaendelea na baadhi ya sehemu zimekamilika zikiwemo maduka, msikiti na uzio wa eneo;

ix. Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Mabasi Malindi; Mfuko umeshapatiwa ruhusa kutoka Serikalini kwa sasa hatua za kusaini mkataba na Mshauri elekezi zimekamilika na mradi huu ndani ya robo ya nne ya mwaka 2023/24 unatarajiwa kuanza; na

x. Kuendelea na Ujenzi wa Soko la Mombasa ambapo mjenzi tayari ameshaanza kazi ya ujenzi wa soko kwa hatua za awali ambazo ni uchimbaji wa msingi na hatua ndogo ndogo ndani ya kipindi cha maandalizi ya ujenzi.

**Shirika la Bima (ZIC)**

**79. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima la Zanzibar lilianzishwa mwezi wa June mwaka 1969 ni miongoni mwa Mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. Kwa hivi sasa Shirika linafanya kazi zake chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina Namba 6 ya mwaka 2021.

**80. Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Shirika yanatokana na vianzio vyake vya mauzo ya Bima pamoja na faida zinazotokana na Uwekezaji, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024, Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 35.1 bilioni** ya mauzo ya Bima ambayo ni sawa na asilimia **87%** ya makadirio ya kukusanya **TZS 40.5 bilioni** katika kipindi cha tathmini. Vile vile Shirika limefanikiwa kupata jumla ya **TZS 620 milioni** ya mapato yanayotokana na Uwekezaji.

**81. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2024, Shirika limetumia jumla ya **TZS 19.6 bilioni** ambapo **TZS 9.6 bilioni** imetumika kulipa madai mbalimbali ya wateja waliopata ajali na

kutimiza matakwa ya Sheria za bima, **TZS 3.1 bilioni** zimetumika kulipa ujira kwa Mawakala na Madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika na **TZS 6.9 bilioni** kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa ofisi.

**82. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi Julai 2023 hadi Machi 2024, Shirika la Bima la Zanzibar imeweza kupata mafanikio yafuatayo: -

i. Shirika limefanikiwa kuzindua huduma mpya za kinga ya bima kwa Wananchi kama ifuatavyo: -

ii. Queen Motor Insurance" Aina ya kinga ya bima mpya na maalumu kwa wanawake;

iii. ZIC Bima Mobile App" ni aina mpya ya bidhaa ya huduma katika soko la bima Tanzania ambapo Shirika linashirikiana na makampuni ya Simu katika kutoa huduma bora za bima kwa Wananchi kwa haraka, usahihi na wakati;

iv. Inbound Travel Insurance". Aina mpya ya huduma ya bima inayotolewa na Shirika kwa wageni hususani watalii wanaofika Zanzibar na Tanzania;

v. Tour Operator Liability Insurance" ni aina mpya ya kinga ya huduma ya bima inayotolewa na Shirika kwa watembeza wageni kwa kuwakinga na majanga;

vi. Shirika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Zanzibar na Tanzania Bara limeweza kutoa taaluma kuhusiana na masuala ya usalama barabarani kwa kuandaa makongamano mbalimbali lengo likiwa ni kupunguza majanga mbalimbali ya ajali;

vii. Shirika limefanikiwa kuongeza wigo wa Biashara ya Bima kwa mashirikiano ya kimkakati na Makampuni na Mabenki mbalimbali katika mfumo wa (Bancassurance) kama vile (VodaBima, Tigo Zantel Bima, Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, DCB Bank, NBC Bank, BOA Bank, Mwalimu Commercial Bank, MUKOBA Bank na PBZ Bank). Lengo ni kuongeza mapato ya Shirika; na

viii. Shirika linaendelea kutoa huduma bora na za kisasa kwa haraka na ufanisi kwa Wananchi kwa kupitia mifumo ya TEHAMA.

**Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

83. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, PBZ imeendelea kukuza mapato yake halisi na kufikia **TZS 131.615 bilioni** ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 ukilinganisha na mapato yaliokadiriwa ya **TZS 124.011 bilioni.** Halikadhalika mapato hayo yaliongezeka kwa asilimia **24** ukilinganisha na mapato ya **TZS 105.753 bilioni** katika kipindi kama hicho cha Julai 2022 hadi Machi 2023. Ongezeko la Mapato kwa kiwango kikubwa kimesababishwa na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo ambayo iliongeza mapato kwa kipindi hicho.

84. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi PBZ imetumia jumla ya TZS 53.947 bilioni ukilinganisha na makadirio ya **TZS 78.633 bilioni** sawa na asilimia **69** kwa kipindi cha tathmini. Aidha, Benki imeweza kuvuka lengo la kupata faida kwa asilimia 71 katika kipindi cha Julai 2023 mpaka Machi 2024 kutoka kiwango kilichokadiriwa cha **TZS 45.377 bilioni** na kufikia **TZS 77.667 bilioni.** Kiwango hiki cha faida ni sawa na ongezeko la asilimia **74** ukilinganisha na faida iliyopatikana katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Machi 2023 ya **TZS 44.722 bilioni.**

85. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 PBZ imefanikiwa kufungua tawi la Amani, vituo vya kutolea huduma vya Uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar (Terminal 3, ambacho kinachotoa huduma kwa masaa 24), Paje, Tunguu na Nungwi, hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa kuwafikia wateja wake katika maeneo muhimu na katika makazi yao.

86. **Mheshimiwa Spika** PBZ ni miongoni mwa walipakodi wakubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Katika kipindi cha miezi tisa Julai 2023 mpaka Machi 2024 imefanikiwa kulipa jumla ya kodi ya **TZS 30.317 billioni** ikiwa ongezeko la

ulipaji wa asilimia 16 ukilinganisha na kiwango cha **TZS 26.212 billioni** iliyolipwa katika kipindi cha Julai 2020 mpaka Machi 2023.

## MASHIRIKIANO NA TAASISI NYENGINE

### Tume ya Pamoja ya Kudumu (JPC)

**87. Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeshiriki vikao vya maandalizi ya Tume ya Pamoja ya Kudumu (JPC) kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Angola vikao ambavyo vinatarajiwa kuanzisha mashirikiano ya pamoja baina ya Tanzania na Angola ambapo pia inatarajiwa kusaini MoU zinazohusu mchakato wa upatikanaji wa Mafuta na Gesi.

### Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji

**88. Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeratibu kikao baina ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kuwasilisha Sera na Sheria za uwekezaji kwa pande zote mbili ili kubadilishana uzoefu katika maeneo husika. Aidha ujumbe huo ulipata bahati ya kutembelea maeneo huru ya uwekezaji Fumba na Nyamanzi. Kwa kushirikiana na Ofisi hii, tunaratibu uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050 kwa pamoja.

### Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania

**89. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imeshirikiana na Wizara ya Fedha katika upatikanaji wa rasilimali fedha za mikopo na misaada kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba, mradi wa afya ya mama na mtoto, ujenzi wa barabara na mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, Ofisi zimeshirikiana katika kuandaa na kuratibu mikutano ya uwili (Bilateral meetings) na mikutano ya kamati za pamoja za ushirikiano kati ya Nchi na Nchi (JPC).

**Kitengo cha udhibiti wa Fedha Haramu (FIU)**

**90. Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa kushirikiana na kitengo cha FIU ilifanikisha kupitia na kuandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria na Kanuni za Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

**MAFANIKIO YA YALIYOPATIKANA**

**91. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miezi tisa Julai hadi Machi ni pamoja na: -

i. Ofisi imeweza kuhamasisha na kupatikana kwa rasilimali fedha za Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa maendeleo ya TZS 504.306 bilioni ili kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya Mahakama, Jinsia, Elimu, Afya, Mawasiliano, Fedha, Maji, Utalii, na Uwezeshaji;

ii. Kuongezeka kwa fedha za Misaada wa Kibajeti (GBS) hadi kufikia TZS 72.965 bilioni kutoka TZS 52.19 kutokana na ushirikishwaji na ufuatiliaji wa karibu wa Ofisi na Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iii. Ofisi kupitia Mamlaka ya Mapato Zanzibar wameimarisha wigo wa kodi kwa kuwasajili walipakodi wapya 4,519;

iv. Ofisi kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanikiwa kutoa mafao mapya kwa wanachama wake, mafao mapya ambayo ni Fao la Kuumia Kazini (Workers Compensation Benefit) na Fao la Upotevu wa Ajira (Unemployment Benefit). Mafao hayo yameongeza imani kwa wanachama dhidi ya Serikali na Mfuko kwa ujumla;

v. Ofisi kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanikiwa kufanya malipo kwa ongezeko la pensheni kutoka TZS 90,000 hadi kufikia TZS 180,000 kuanzia mwezi Julai 2023; na

vi. Uratibu wa kifedha kufanikisha miradi ya kimkakati ikiwemo masoko (Jumbi,Mwanakwerekwe na Chuini) na uwanja wa michezo "New Amaan Complex"ambapo miradi hii tayari imekemilika.

**CHANGAMOTO**

**92. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miezi tisa Julai hadi Machi 2023/24, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango katika kutekeleza majukumu yake ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Ingawa kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya kodi bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, hawatumii mashine ya kielekroniki na wananchi wengi bado hawana muamko wa kudai risiti;

ii. Upungufu mkubwa wa fedha za kigeni hususan Dola ya Marekani hali iliopelekea kuathiri sana biashara, hasa kwa wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka nje ya nchi; na

iii. Mfumo wa BAMAS haujaweza kubeba baadhi ya moduli. Hivyo, mchakato wa marekebisho unasababisha kutokuanza kutumika mfumo huu kwa Taasisi zote mara moja.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO**

**93. Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto tulizozielezea Ofisi inaendelea kuweka mikakati madhubuti kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo ikiwemo: -

i. Mamlaka ya Mapato (ZRA) imekuwa ikichukua jitihada za kuwafuatilia wafanyabiashara wasiotowa risiti na kuwapa adhabu kwa mujibu wa sheria pamoja na kutoa elimu ya kutoa na kudai risiti;

ii. Benki Kuu Tanzania (BoT) imechukua juhudi mbali mbali kuhakikisha inaimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni kwa uhakika; na

iii. Ofisi kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao ipo katika hatua ya maboresho ya baadhi ya moduli ili mfumo (BAMAS) huo uweze kutumika kama ilivyopangwa.

## F. MWELEKEO WA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024-2025

### Vipaumbele vya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango

**94. Mheshimiwa Spika,** Bajeti hii imezingatia Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050, Mpango Mkakati wa Maendeleo (ZADEP), Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 na Hotuba ya Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi siku ya tarehe 11/11/2020 pamoja maagizo mbali mbali ya Mheshimiwa Rais. Pamoja na mwenendo wa hali ya uchumi na teknolojia ya mifumo ya kielektroniki katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti upotevu wa mapato, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango imejipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Serikali;

ii. Kusimamia na kutekeleza Bajeti yenye kuzingatia Jinsia;

iii. Kuandaa Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) kuhusu Uanzishaji wa Soko la Hisa (Zanzibar Stock Exchange); pamoja na Benki ya Uwekezaji Zanzibar (Zanzibar Investment Bank);

iv. Kuanza maandalizi ya kuanzisha Chuo cha Usimamizi wa Fedha (Chwaka);

v. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara wadogo wadogo pamoja na ukusanyaji wa mapato katika Masoko Mapya;

vi. Kuimarisha usimamizi wa Sera na Kada ya Ununuzi;

vii. Kuimarisha usimamizi wa Mali za Umma kwa kukamilisha mfumo wa ZGAMIS;

viii. Kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Muda wa Kati wa Mpango wa Maendeleo (ZADEP 2021-2026) na Kuanza maandalizi ya Mkakati mpya wa Maendeleo wa muda wa kati Zanzibar;

ix. Kuimarisha Modeli za kuichumi (Macroeconomic Model) na kuanzisha modeli mpya ya utabiri wa uchumi (Projection Dynamic Economic model);

x. Kuandaa sera ya viashiria vya kiuchumi (Macroeconomic Policy Framework);

xi. Kufanya na kuratibu tafiti nne (4) na maandiko mafupi ya Sera 10 (Policy Brief) za kimkakati kulingana na vipaumbele vya tafiti vya taifa;

xii. Kuandaa Kanzidata ya vipaumbele vya ujuzi vya Taifa (National Skills Database) ambayo itatoa fani tulizonazo katika soko la ajira na fani zinazohitajika pamoja na mfumo wa kuwatambua wahitimu wa elimu ya juu Zanzibar;

xiii. Kutumia Mfumo wa "Geographical Information System" ambao utasaidia kutupatia takwimu na picha za matokeo sahihi zaidi za kisekta zinazohusiana na maendeleo ya wananchi ; na

xiv. Kukamilisha Programu za miradi iliyoanza miaka iliyopita.

**95. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa dhamira ya kuimarisha utendajiwa kazi, ilianzisha Idara mpya mbili (2) ambazo ni Idara ya Huduma za Sheria na Idara ya Usimamizi wa Sera za Ununuzi wa Umma.

**96. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Sheria ina jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mikataba na sheria mbalimbali zilizo chini ya Ofisi pamoja na mienendo ya kesi ambazo ofisi imeshtaki au kushtakiwa. Idara pia inajukumu la kisimamia mikataba na kutoa ushauri katika vipengele mbalimbali vya mikataba.

97. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Usimamizi wa Sera za Ununuzi wa umma ina jukumu la kuandaa na kusimamia Sera,Sheria, kanuni na miongozo inayohusiana na ununuzi wa umma na kuishauri Serikali katika masuala yanayohusu ununuzi wa umma pamoja na kusimamia Kada ya ununuzi wa umma. Mheshimiwa Spika, Hivyo, Bajeti hii itajumuisha matumizi ya idara hizi mbili.

98. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza vipaumbele vya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, naomba kuwasilisha mwelekeo wa mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

**Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango**

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inakadiriwa kukusanya **TZS 4,901.7 bilioni.** Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia **77** ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya **TZS 2,767.8 bilioni** yaliyopangwa kukusanywa kwa mwaka 2023/2024.

100. **Mheshimiwa Spika,** Mapato hayo yamekadiriwa kukusanywa katika mafungu ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kama ifuatavyo:

i. Fungu F01 limekadiriwa kukusanya TZS 2,981.083 bilioni;

ii. Fungu F04 limekadiriwa kukusanya TZS 0.134 bilioni;

iii. Fungu F05 limekadiriwa kukusanya TZS 1,884.5 bilioni; na

iv. Fungu F07 limekadiriwa kukusanya TZS 35.959 bilioni.

101. **Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa mapato hayo kwa vyanzo unaonekana katika kiambatanisho namba 3.

**Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango.**

102. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 1,133.21 bilioni** kwa mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango na uchambuzi wake ni:

i. Fungu F01 imekadiriwa kutumia TZS 665.392 bilioni;
ii. Fungu F02 imekadiriwa kutumia TZS 416.897 bilioni;
iii. Fungu F03 imekadiriwa kutumia TZS 11.767 bilioni;
iv. Fungu F04 imekadiriwa kutumia TZS 13.113 bilioni;
v. Fungu F05 imekadiriwa kutumia TZS 14.754 bilioni;
vi. Fungu F06 imekadiriwa kutumia TZS 6.069 bilioni; na
vii. Fungu F07 imekadiriwa kutumia TZS 5.219 bilioni.

**103. Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa hizo za mafungu naomba kuwasilisha uchambuzi wa matumizi ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kila fungu kama ifuatavyo:-

**Matumizi kwa Fungu F01**

**104. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu F01 yanakadiriwa kufikia TZS 665.392 bilioni. Kati ya fedha hizo, **TZS 134.771 bilioni** ni mishahara (**TZS 130.665 bilioni** kwa ajili ya marekebisho ya mishahara), **TZS 36.102 bilioni** matumizi ya kawaida (kati ya fedha hizo TZS 11.102 bilioni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **TZS 25 bilioni** ni fedha za ununuzi wa gari kwa Taasisi zinazojitegemea), TZS 30.612 bilioni Ruzuku za Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango, na **TZS 463.907 bilioni f**edha za miradi ya maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma imekadiriwa TZS 161.755 bilioni;

ii. Programu ya Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Masuala ya Sheria imekadiriwa TZS 4.438 bilioni;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imekadiriwa TZS 499.198 bilioni;

### Matumizi kwa fungu F02

105. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu F02 yanakadiriwa kufikia **TZS 416.897 bilioni** Kati ya fedha hizo, **TZS 2.792 bilioni** Mshahara, **TZS 414.105 bilioni** matumizi ya kazi za kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali.

### Matumizi kwa fungu F03

106. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi kwa fungu F03, yanakadiriwa kufikia TZS 11.766 bilioni, Kati ya fedha hizo **TZS 2.288 bilioni** Mshahara, **TZS 4.178 bilioni** matumizi ya kazi za kawaida na **TZS 5.300 bilioni** Matumizi ya kazi za Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

   i. Programu ya Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini Programu imekadiriwa TZS 7.380 bilioni;

   ii. Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti imekadiriwa kutumia TZS 1.585 bilioni; na

   iii. Programu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango imekadiriwa kutumia TZS 2.801 bilioni.

### Matumizi kwa Fungu F04

107. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi kwa fungu F04, yanakadiriwa kufikia TZS 13.113 bilioni, Kati ya Fedha hizo, **TZS 2.352 bilioni** Mshahara, **TZS 2.099 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida na **TZS 8.662 bilioni** kwa ajili ya Kazi za Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

   i. Programu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii TZS 8.932 bilioni; na

   ii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali TZS 4.181 bilioni.

**Matumizi kwa Fungu F05**

**108. Mheshimiwa Spika,** Matumizi kwa fungu F05, yanakadiriwa kufikia **TZS 14.754 bilioni,** Kati ya Fedha hizo, **TZS 11.378 bilioni** Mshahara, **TZS 3.376 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma TZS 1.090 bilioni; na

ii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali TZS 13.664 bilioni.

**Matumizi kwa Fungu F06**

**109. Mheshimiwa Spika,** Matumizi kwa Fungu F06, yanakadiriwa kufikia **TZS 6.069 bilioni,** kati ya Fedha hizo, **TZS 4.214 bilioni** Mshahara, **TZS 1.855 bilioni** Matumizi ya Kazi za Kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Huduma za Ukaguzi na Ushauri TZS 825.290 milioni; na

ii. Programu ya Utawala na Uendeshaji TZS 5.244 bilioni.

**Matumizi kwa Fungu F07**

**110. Mheshimiwa Spika,** Matumizi kwa fungu F07 yanakadiriwa kufikia **TZS 5.219 bilioni,** Kati ya fedha hizo, **TZS 936.0 milioni** Mshahara na TZS 4.282 bilioni matumizi ya kazi za kawaida. Fedha hizi zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu zifuatazo: -

i. Programu ya Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma TZS 3.367 bilioni; na

ii. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina TZS 1.851 bilioni.

**111. Mheshimiwa Spika,** pamoja na programu kuu zilizowasilishwa, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango itatekeleza programu ndogo Thelathini na Sita (36) ambazo uchambuzi wake unaonekana katika **kiambatisho namba 4.**

**Matumizi ya Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais -Fedha na Mipango kwa Mwaka 2024/2025**

**112. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa Mwaka 2024/2025 imelenga kutekeleza programu na miradi ya maendeleo yenye thamani ya **TZS 477.869 billioni** kama ifuatavyo: -

**Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)**

**113. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuimarisha Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili. Fedha za mradi huu ni Mkopo nafuu kutoka kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu unakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 1.065 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 986.878 milioni** ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo (AfDB) na **TZS 78.500 milioni** mchango kutoka SMZ.

**Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z).**

**114. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalenga kuimarisha hali ya Maisha na Kukuza Maendeleo ya Kiuchumi katika Maeneo ya Miji ya Zanzibar, fedha za Programu hii ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 32 bilioni** ili kukamilisha miradi mbali mbali.

**Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP IV).**

**115. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalenga kuleta Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma, fedha za programu hii ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 inakadiriwa

kutumia Jumla ya **TZS 4.858 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 4.458 bilioni** ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo na **TZS 400 milioni** mchango kutoka SMZ.

**Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali**

**116. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalengo la kuimarisha Ofisi za Serikali, inatekelezwa kwa fedha za SMZ. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii inakadiriwa kutumia kiasi **TZS 113.983 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 80.261 bilioni** ni fedha za mradi wa ukamilishaji wa Ofisi za Serikali na **TZS 33.722 bilioni** fedha za mradi wa Ujenzi wa Mji wa Serikali.

**Ulipaji wa madeni kwa Miradi ya Maendeleo**

**117. Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imetenga fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni kwa miradi ya maendeleo kwa makadirio ya **TZS 312.0 bilioni.**

**Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar**

**118. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2024/2025, Programu hii inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 3.0 bilioni** kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**Mradi wa Mapitio, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, VISION 2050, SDGs na AFRICAN AGENDA)**

**119. Mheshimiwa Spika,** Mradi una lengo la kuimarisha Uratibu, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, mradi huu unakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 2.3 bilioni** kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**Mradi wa Uendelezaji Takwimu (ZSDP)**

**120. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kupitia Bajeti ya kazi za Maendeleo inaendelea na Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Uimarishaji wa Takwimu Awamu ya Pili (TSMP II) ambao umelenga kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar hususani kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati; kuweka mazingira mazuri ya kuratibu upatikanaji wa viashiria na takwimu za Kiuchumi na Kijamii kupitia Takwimu za kawaida, Sensa na tafiti. Mpango huu utekelezaji wake ni wa miaka mitano 2022/2023 hadi 2026/2027 na umelenga kuwezesha Uzalishaji na Usimamizi wa Takwimu, Uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, Maendeleo ya Rasilimali Watu kwa Taasisi za kiserikali kupitia Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kusaidia uimarishaji na upatikanaji wa Takwimu rasmi. Mpango huu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 umekadiriwa kutumia **TZS 8.662 bilioni.**

**121. Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango unaonekana katika kiambatisho namba 5.

**MWELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO 2024/2025**

**Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

**122. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Mamlaka ya Mapato ZRA imekadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 845.979 bilioni** sawa na asilimia **25** ya ongezeko la makadirio ya **TZS 675.601 bilioni** kwa mwaka wa Fedha 2023/24. ZRA pia imekadiriwa kupokea ruzuku kutoka Serikalini jumla ya **TZS 26.168 bilioni.**

**Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

**123. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar imekadiriwa

kukusanya Jumla ya **TZS 600.082 bilioni** ni sawa na ongezeko la asilimia **15** ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2023/2024 ambayo yalikuwa ni **TZS 520.640 bilioni.**

**Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA) Mapato**

**124. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imekadiria kukusanya TZS 989.0 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.

***Matumizi***

**125. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, imekadiriwa jumla ya **TZS 2.953 bilioni** ambayo ni Ruzuku kutoka Serikalini kati ya fedha hizo **TZS 1.708 bilioni** kwa ajili ya ulipaji wa mishahara na **TZS 1.245 bilioni** kwa kutekeleza shughuli za ofisi zilizopangwa. Mamlaka itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na kutarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kukamilisha mpango wa kutunga sheria mpya;

ii. Kufanya ukaguzi wa ununuzi kwa Taasisi nunuzi (60) na uchunguzi wa ununuzi kwa Taasisi nunuzi (8);

iii. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba kwa Taasisi (20);

iv. Kufanya mafunzo ya Sheria, kanuni na miongozo ya Ununuzi wa Umma kwa maafisa manunuzi 100, Maafisa masuuli 140 na wajumbe wa Bodi za Zabuni 163;

v. Kuandaa miongozo mitatu 3 ya manunuzi;

vi. Kufanya mafunzo juu ya kujibu zabuni kwa watoa huduma 280;

vii. Kufanya mafunzo juu ya ununuzi wa bidhaa, kazi na ushauri usio wa kitaalam na usimamizi wa mikataba kwa maafisa ununuzi 150; na

viii. Kufanya mkutano wa mwaka na wadau wa ununuzi kwa washiriki 180.

### Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

#### *Mapato*

126. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 unatarajia kukusanya jumla ya **TZS. 323.36 billioni** kutoka katika vyanzo vikuu viwili ambavyo ni **TZS 199.64 bilioni** michango ya wanachama na **TZS 123.72 bilioni** mapato ya uwekezaji.

#### *Matumizi*

127. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi Mfuko unatarajia kufanya malipo ya mafao, usimamizi wa miradi na uwekezaji na gharama za uendeshaji kwa kiasi cha **TZS 323.35 bilioni** kwa matumizi yake ya mwaka 2024/2025. Kati ya hizo **TZS 15.45 billioni** kwa ajili ya gharama za uendeshaji, **TZS 103.58 billioni** kwa ajili ya Mafao na **TZS. 204.32 billioni** kwa ajili ya usimamizi wa miradi na uwekezaji.

### Mikakati ya kufikia Malengo

128. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utekelezaji wa majukumu ya kawaida, Mfuko pia umepanga mikakati ifuatayo: -

i. Kuendeleza na kuimarisha mashirikiano na taasisi za Serikali kwa lengo la kuimarisha usajili wa wanachama na kuwasilisha michango na pia kusaidia ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

ii. Kufanya miradi midogo midogo yenye tija kubwa na maslahi ya moja kwa moja kwa wananchi na Mfuko kwa ujumla;

iii. Kuendelea kufanya uwekezaji wa fedha kwa kipindi cha muda mfupi na muda mrefu katika hatifungani, hatifungate, uwekezaji katika mabenki na kuendelea kutoa mikopo kwa Serikali, mashirika, taasisi na kampuni binafsi yenye tija katika Mfuko;

iv. Kusimamia uwekezaji wa majengo kwa kuhakikisha kuwa malipo yanalipwa kwa wakati, mikataba inasainiwa na hali ya majengo inaendelea kuwa vizuri; na

v. Kuanzisha rasmi utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa kuzingatia misingi ya Sheria za Kiislam.

**Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

**129. Mheshimiwa Spika,** Malengo ya PBZ kwa mwaka 2024 Katika kutekeleza bajeti yake inakadiria kufikia viwango vifuatavyo:-

***Mapato***

**130. Mheshimiwa Spika,** Mapato ya benki kuongezeka kwa asilimia **38** kutoka **TZS. 154.784 bilioni** na kufikia **TZS 214.079 bilioni.**

***Matumizi***

**131. Mheshimiwa Spika,** Matumizi yanakadiriwa kuongezeka kutoka **TZS 80.721 bilioni** na kufikia **TZS. 118.141 bilioni,** ikiwa ni ongezeko la asilimia 46. Aidha, PBZ imekadiria kupata faida ya **TZS 95.938 bilioni** ikiwa ni ongezeko la asilimia **30** ukilinganisha na faida halisi ilioipata ya **TZS 74.063 bilioni** katika mwaka 2023.

i. Rasilimali za benki zinakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 27 na kufikia TZS 2.605 trilioni ukilinganisha na rasilimali za TZS 2.051 trilioni zilizorekodiwa mwaka 2023;

ii. Amana za wateja zinatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 35 na kufikia TZS 2.162 trilioni ukilinganisha na amana za TZS 1.607 trilioni zilizopatikana mwishoni mwa bajeti ya mwaka 2023;

iii. Jumla ya mikopo ya kawaida na inayofuata sharia ya kiislam imekadiriwa kukuwa kwa asilimia 27 kutoka TZS 1.038 trilioni iliyofikiwa mwaka 2023 na kufikia TZS 1.318 trilioni kwa mwaka 2024; na

iv. Mtaji wa benki umekadiriwa utafikia TZS 226.805 bilioni kwa mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 28 ukilinganisha na mtaji uliofikiwa mwaka 2023 wa TZS 176.855 bilioni.

**Mikakati ya kuboresha huduma**

**132. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 PBZ imejipanga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i. Ufunguzi wa matawi mapya katika mikoa ya Mbeya na Morogoro;

ii. Kuanza ujenzi wa matawi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Tanga;

iii. Ujenzi wa vituo vya kutolea huduma (service centres) kwa Pemba (maeneo ya ZSTC Madungu na Konde), Unguja (Kiwengwa na Kinyasini), na Dar-es-salaam (Ubungo, Bandarini (TPA) na Mbagala);

iv. Kuweka mashine za kutolea fedha (ATM) katika maeneo ya Machomane, Jumbi, Mwera, Fumba, Kombeni, Kwa nyanya (kituo cha mabasi) na Mkokotoni; na

v. Kuboresha miundombinu ya TEHAMA kwa kununua switchi yake (Financial Switch) ambayo itarahisisha na kuiongezea mapato benki kwenye huduma za mashine za kutolea fedha (ATM), vile vile inategemea kuzindua mfumo wa kisasa wa benki kiganjani (mobile application).

**Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC)**

***Mapato***

**133. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima kwa mwaka fedha 2024/25 linatarajia kukusanya jumla ya **TZS 54.2 bilioni k**utoka katika vianzio vyake vya mapato kwa kutekeleza mikakati ifuatayo: -

i. Kutoa taaluma na kujitangaza kwa Wananchi na Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja wapya wa biashara zisizokuwa za magari katika mtandao wake;

ii. Kuzidisha mashirikiano baina ya mawakala na madalali wanaofanya baishara ya kuuza bima kwa niaba ya Shirika;

iii. Shirika kuendelea kushirikiana kikamilifu na mabenki mbalimbali katika mfumo wa "Bancassurance" kwa lengo la kuongeza mapato yake;

iv. Kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kuhakikisha Miradi yote mikubwa ya Maendeleo kwa Wananchi inakatiwa kinga za Bima na Shirika; na

v. Shirika kuendelea kufanya ubunifu wa uzinduzi wa huduma mpya mbalimbali za Bima kwa Wananchi kwa lengo la kupata wateja wapya pamoja na kuongeza mapato yake.

***Matumizi***

134. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Shirika kwa mwaka wa fedha 2024/25 limekadiriwa kutumia jumla ya TZS 30.7 bilioni ikijumuisha matumizi yafuatayo:

i. Matumizi kwa kazi za kawaida za Shirika ''Management Expenses" ni TZS 13.3 bilioni;

ii. Matumizi ya ununuzi wa vitendea kazi kwa matumizi ya watendaji wa Shirika ni TZS 2.5 bilioni, ikijumisha ununuzi wa samani za ofisi, ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Tehama, pamoja na ununuzi wa magari mawili mapya kwa matumizi ya ofisi za Shirka;

iii. Matumizi ya malipo ya madai kwa wateja watakaoathirika na majanga mbalimbali ya ajali TZS 11.0 bilioni; na

iv. Matumizi ya malipo ya ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya kazi ya kuuza Bima kwa niaba ya Shirika TZS 3.9 bilioni.

**Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT)**

***Mapato***

135. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ZIAAT inatarajia kukusanya jumla ya **TZS 174.92 milioni** kutoka kwenye

vianzio vyake vya mapato ambavyo ni Ada ya Usajili, Ada ya Utambuzi, Ada ya Leseni, Ada ya Mwaka ya Uanachama na Ada ya Mafunzo.

***Matumizi***

**136. Mheshimiwa Spika,** Katika kuyafikia malengo yaliyowekwa na Taasisi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ZIAAT imepangiwa kutumia **TZS 1.49 bilioni.** Kati ya fedha hizo **TZS 270 milioni** kwa ajili ya Mishahara na **TZS 1.22 bilioni** kwa kazi za Uendeshaji wa Ofisi zikiwemo:

i. Kuandaa Mitaala ya Mitihani ya Kodi pamoja na Miongozo ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar; na

ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi, kufanya ziara za kimafunzo kwa Wajumbe wa Bodi na Wafanyakazi kwa lengo la kubadilishana mawazo na kupata uelewa kwa Taasisi zinazofanana na ZIAAT.

## G. HITIMISHO

**137. Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti na wajumbe wa Baraza lako kwa ushauri na miongozo yenu mnayotupatia katika utendaji wa shughuli zetu. Nawashukuru pia, Viongozi na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango pamoja na Viongozi wa Taasisi zetu zote zinazojitegemea kwa mashirikiano yao katika kukamilisha taarifa hii ambayo leo tunaiwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi.

**138. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inawaomba wajumbe wa Baraza lako kupokea, kujadili na hatimae kuikubali taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato ya jumla ya **TZS 4,901.7 bilioni** na matumizi ya kawaida na maendeleo ya jumla ya **TZS 1,133.21 bilioni** ili kufanikisha shughuli ilizojipangia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**139. Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

**Dkt. SAADA MKUYA SALUM,**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**

## H. VIAMBATANISHO

*Jadweli Namba: 1 Muhtasari wa Mapato kwa Kipindi cha Julai – Machi, 2023/24*

| VIANZIO | Makisio ya Mwaka 2023/2024 | Makisio Julai - Machi 2023/2024 | Makusanyo halisi kwa kipindi cha Julai - Machi 2023/2024 | Asilimia ya Makusanyo kwa kipindi cha Julai-Machi 2023/24 | Asilimia ya Makusanyo kwa kipindi cha Mwaka 2023/24 |
|---|---|---|---|---|---|
| **MAPATO FO1** | | | | | |
| **MAPATO YA KODI** | | | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 520,643,979,000 | 383,978,498,526 | 384,366,649,604 | 100 | 74 |
| ZRA | 675,601,261,068 | 479,178,758,759 | 559,484,054,483 | 117 | 83 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,196,245,240,068** | **863,157,257,284** | **943,850,704,087** | **109** | **79** |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA ODA | 634,426,593,000 | 475,819,944,750 | 504,306,174,111 | 106 | 79 |
| **JUMLA NDOGO** | **634,426,593,000** | **475,819,944,750** | **504,306,174,111** | **106** | **79** |
| **MAPATO YASIO KUWA YA KODI** | | | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 35,000,000,000 | 1,445,498,000 | 150,000,000 | 10 | 0 |
| KODI YA BOHARI | 1,065,399,000 | 778,000,000 | 131,977,000 | 17 | 12 |
| UHAMIAJI | 75,000,000,000 | 60,161,255,905 | 66,875,760,687 | 111 | 89 |
| **JUMLA NDOGO** | **111,065,399,000** | **62,384,753,905** | **67,157,737,687** | **108** | **60** |
| **MAPATO MENGINEYO YASIYOKUWA YA KODI** | | | | | |
| UUZAJI WA VIFAA VIKONGWE | 2,360,018,000 | 1,812,393,500 | 711,318,600 | 39 | 30 |
| KODI YA MAJENGO ZINAZOSIMAMIWA NA ORFM | 913,199,000 | 605,200,000 | 49,716,000 | 8 | 5 |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | 22,830,000 | 17,130,000 | 9,707,000 | 57 | 43 |
| ADA YA MATUMIZI YA NYARAKA | 450,000,000 | 135,000,000 | 172,800,112 | 128 | 38 |
| MATANGAZO | 70,000,000 | 37,500,000 | 22,810,000 | 61 | 33 |
| USAJILI WA WAZABUNI | 180,000,000 | 15,000,000 | 144,695,355 | 965 | 80 |
| ADA YA MAFUNZO | 50,000,000 | 50,000,000 | 23,320,000 | 47 | 47 |
| **JUMLA NDOGO** | **4,046,047,000** | **2,672,223,500** | **1,134,367,067** | **42** | **28** |
| **JUMLA F01** | **1,945,783,279,068** | **1,404,034,179,439** | **1,516,448,982,952** | **108** | **78** |
| **MAPATO F04** | | | | | |
| VIBALI VYA UTAFITI | 64,750,000 | 44,002,833 | 45,270,750 | 103 | 70 |
| UKODISHWAJI WA KUMBI ZA MIKUTANO | 35,250,000 | 27,472,000 | 21,750,000 | 79 | 62 |
| KUTOA USHAURI ELEKEZI JUU YA MASUALA YA TAFITI | 20,000,000 | 15,820,000 | 4,560,000 | 29 | 23 |
| **JUMLA F04** | **120,000,000** | **87,294,833** | **71,580,750** | **82** | **60** |
| **MAPATO F05** | | | | | |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI (PAYE) | 21,000,000,000 | 15,750,000,000 | 14,000,000,000 | 89 | 67 |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 8,400,000,000 | 6,300,000,000 | 6,300,000,000 | 100 | 75 |
| MABUKU NA STAKABADHI | 35,972,850 | 26,772,850 | 15,118,840 | 56 | 42 |
| MCHANGO KUTOKA TAASISI YA VIWANGO (ZBS) | 2,400,000,000 | 1,800,000,000 | - | - | - |
| MCHANGO KUTOKA BPRA | 480,000,000 | 360,000,000 | 360,000,000 | 100 | 75 |
| MCHANGO KUTOKA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI | 1,920,000,000 | 1,440,000,000 | 1,280,000,000 | 89 | 67 |
| MCHANGO KUTOKA KAMISHENI YA UTALII | 4,800,000,000 | 3,600,000,000 | 1,176,307,888 | 33 | 25 |
| HATI FUNGANI | 150,000,000,000 | 150,000,000,000 | 108,840,729,956 | 73 | 73 |
| MKOPO KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO | 567,210,000,000 | 567,210,000,000 | 487,790,096,000 | 86 | 86 |
| GAWIO LA BOT | 13,500,000,000 | 13,500,000,000 | 4,500,000,000 | 33 | 33 |
| MISAADA YA KIBAJETI (GBS/URT) | 52,190,000,000 | 35,000,000,000 | 72,965,660,398 | 208 | 140 |
| **JUMLA F05** | **821,935,972,850** | **794,986,772,850** | **697,227,913,082** | **88** | **85** |
| **JUMLA KUU** | **2,767,839,251,918** | **2,199,108,247,122** | **2,213,748,476,784** | **101** | **80** |

*Jadweli Namba: 2 Matumizi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Julai – Machi, 2023/24 (Tarakimu milioni)*

| Programu Kuu | Programu ndogo | Makisio Mwaka (2023-2024) | Makisio Julai - Machi 2023/2024 | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Julai-Machi 2023-2024 | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Mwaka 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | SMZ | Mhisani | | | | |
| Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | 1,091.13 | 927.87 | 587.51 | 206.11 | | 96.49 | | 890.10 | **96** | **82** |
| | Marekebisho ya Mishahara | 86,086.76 | 86,086.76 | 86,086.76 | | | | | 86,086.76 | **100** | **100** |
| | Uratibu wa Fedha za Nje | 981.45 | 703.70 | 217.05 | 1,264.84 | | | | 1,481.89 | **211** | **151** |
| | Fedha na Sera za Kodi | 37,891.42 | 30,175.69 | 270.32 | 48.20 | | | 27,445.17 | 27,763.68 | **92** | **73** |
| | mifumo ya udhibiti na usimamizi wa fedha za umma | 652.95 | | | | | | | - | | **-** |
| | **Jumla ndogo** | **126,703.71** | **117,894.02** | **87,161.63** | **1,519.14** | | **96.49** | **27,445.17** | **116,222.42** | **99** | **92** |
| Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | Mitaji ya Umma | 80,217.67 | 15,318.14 | 595.32 | 1,386.01 | 5,652.89 | | 1,630.49 | 9,264.71 | **60** | **12** |
| | Usimamizi wa ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali | 198.35 | | | | | | | | | **-** |
| | **Jumla ndogo** | **80,416.02** | **15,318.14** | **595.32** | **1,386.01** | **5,652.89** | **-** | **1,630.49** | **9,264.71** | **60** | **12** |
| Uendeshaji na uratibu wa wizara ya Fedha na Mipango | Utumishi na Uendeshaji | 5,695.01 | 5,313.02 | 1,587.40 | 9,950.97 | | | | 11,538.37 | **217** | **203** |
| | Mipango, Sera na Utafiti | 173,389.87 | 10,162.92 | 157.24 | 39.33 | 3.33 | 3,324.09 | | 3,523.98 | **35** | **2** |
| | Ofisi kuu Pemba | 2,568.62 | 2,024.18 | 542.03 | 440.00 | | | | 982.03 | **49** | **38** |
| | **Jumla ndogo** | **181,653.50** | **17,500.13** | **2,286.66** | **10,430.29** | **3.33** | **3,324.09** | | **16,044.37** | **92** | **9** |
| | **Jumla F01** | **388,773.23** | **150,712.28** | **90,043.61** | **13,335.44** | **5,656.22** | **3,420.58** | **29,075.65** | **141,531.50** | **94** | **36** |
| Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 258,449.40 | 202,114.13 | | 214,955.05 | | | | 214,955.05 | **106** | **83** |
| | **Jumla ndogo** | **258,449.40** | **202,114.13** | | **214,955.05** | | | | **214,955.05** | **106** | **83** |
| | **Jumla F02** | **258,449.40** | **202,114.13** | **-** | **214,955.05** | **-** | **-** | **-** | **214,955.05** | **106.3533031** | **83.17103812** |
| Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi | Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini | 4,419.16 | 3,184.46 | 165.24 | 70.71 | 911.91 | | | 1,147.86 | **36** | **26** |
| | Maendeleo ya Watendakazi wa Masuala ya Idadi ya Watu | 871.21 | 637.54 | 191.15 | 66.38 | | | | 257.53 | **40** | **30** |
| | Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo | 2,469.46 | 1,989.52 | 266.83 | 90.50 | | | | 357.32 | **18** | **14** |
| | **Jumla ndogo** | **7,759.83** | **5,811.52** | **623.21** | **227.58** | **911.91** | | | **1,762.71** | **30** | **23** |
| Usimamizi wa Uchumi Mkuu | Usimamizi wa Uchumi Mkuu | 405.96 | 320.66 | 189.44 | 59.14 | | | | 248.58 | **78** | **61** |
| | Utafiti | 964.32 | 872.93 | 114.95 | 140.28 | | | | 255.23 | **29** | **26** |
| | **Jumla ndogo** | **1,370.28** | **1,193.59** | **304.39** | **199.42** | | | | **503.80** | **42** | **37** |
| Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | 1,610.79 | 1,244.54 | 507.97 | 465.13 | | | | 973.10 | **78** | **60** |
| | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Pemba | 426.11 | 318.93 | 225.22 | 52.80 | | | | 278.02 | **87** | **65** |
| | **Jumla ndogo** | **2,036.90** | **1,563.47** | **733.18** | **517.93** | | | | **1,251.12** | **80** | **61** |
| | **Jumla F03** | **11,167.01** | **8,568.58** | **1,660.78** | **944.93** | **911.91** | **-** | **-** | **3,517.63** | **41.05264357** | **31.50019003** |
| Kuendeleza na kuratibu Takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii | Ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii | 4,758.32 | 1,070.79 | 786.87 | 125.27 | | 804.09 | | 1,716.24 | **160** | **36** |
| | Uratibu wa shughuli za Kitakwimu katika mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar | 1,217.50 | 324.74 | 206.36 | 38.90 | | 424.02 | | 669.27 | **206** | **55** |
| | **Jumla ndogo** | **5,975.82** | **1,395.53** | **993.23** | **164.17** | | **1,228.11** | | **2,385.51** | **171** | **40** |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Utawala na Uendeshaji Unguja | 1,659.12 | 1,156.51 | 410.53 | 207.23 | - | 85.78 | | 703.53 | **61** | **42** |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba | 631.52 | 327.24 | 244.88 | 15.15 | - | | | 260.03 | **79** | **41** |
| | **Jumla ndogo** | **2,290.64** | **1,483.75** | **655.41** | **222.37** | | **85.78** | | **963.56** | **65** | **42** |
| | **Jumla F04** | **8,266.46** | **2,879.28** | **1,648.64** | **386.55** | **-** | **1,313.89** | **-** | **3,349.07** | **116.3162318** | **40.5139515** |

*Jadweli namba 2 linaendelea.*

| Programu Kuu | Programu ndogo | Makisio Mwaka (2023-2024) | Makisio Julai - Machi 2023/2024 | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Julai-Machi 2023-2024 | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Mwaka 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | SMZ | Mhisani | | | | |
| Usimammizi wa Hazina | Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali yasiyokuwa ya Kodi | 111.18 | 84.15 | | 23.57 | | | | 23.57 | **28** | **21** |
| | Kusimamia ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali | 46.44 | 46.44 | | 14.19 | | | | 14.19 | **31** | **31** |
| | Usimamizi wa Matumizi ya Serikali | 143.15 | 118.66 | | 59.61 | | | | 59.61 | **50** | **42** |
| | Usumamizi wa Deni la Taifa | 363.54 | 269.15 | | 78.05 | | | | 78.05 | **29** | **21** |
| | **Jumla ndogo** | **664.30** | **518.40** | | **175.42** | | | | **175.42** | **34** | **26** |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Uratibu wa Mipango | 335.63 | 147.03 | | - | | | | | **-** | **-** |
| | Utawala na Uendeshaji Unguja | 7,928.52 | 8,010.79 | 6,122.60 | 542.17 | | | | 6,664.77 | **83** | **84** |
| | Utawala na Uendeshaji Pemba | 2,213.55 | 2,125.75 | 1,905.98 | 68.73 | | | | 1,974.71 | **93** | **89** |
| | **Jumla ndogo** | **10,477.70** | **10,283.57** | **8,028.58** | **610.90** | | | | **8,639.48** | **84** | **82** |
| | **Jumla F05** | **11,142.00** | **10,801.97** | **8,028.58** | **786.32** | | | | **8,814.90** | **81.60455917** | **79.11416263** |
| Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa kamati za Ukaguzi na Taarifa jumuishi za ukaguzi wa ndani | 63.83 | 63.83 | | | | | | | **-** | **-** |
| | Uchunguzi wa Ubadhirifu na vihatarishi | 121.28 | 99.17 | | 25.26 | | | | 25.26 | **25** | **21** |
| | Usimamizi wa uthibitisho wa ubora | 25.51 | 24.14 | | 7.85 | | | | 7.85 | **33** | **31** |
| | **Jumla ndogo** | **210.62** | **187.13** | | **33.11** | | | | **33.11** | **18** | **16** |
| Utawala na Uendeshaji | Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango,Mafunzo na Utafiti | 4,162.61 | 3,161.69 | 3,256.34 | 456.89 | | | | 3,713.23 | **117** | **89** |
| | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Ofisi Pemba | 825.48 | 620.01 | 753.81 | 28.61 | | | | 782.42 | **126** | **95** |
| | **Jumla ndogo** | **4,988.10** | **3,781.70** | **4,010.15** | **485.50** | | | | **4,495.65** | **119** | **90** |
| | **Jumla F06** | **5,198.71** | **3,968.83** | **4,010.15** | **518.61** | | | | **4,528.76** | **114.1081196** | **87.11300278** |
| | **JUMLA KUU** | **682,996.81** | **379,045.07** | **105,391.76** | **230,926.90** | **6,568.13** | **4,734.47** | **29,075.65** | **376,696.91** | **99** | **55** |

*Jadweli Namba: 3 Muhtasari wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/25*

| VIANZIO | MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | ASILIMIA YA ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| **MAPATO FO1** | | | |
| **MAPATO YA KODI** | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 520,640,979,000 | 600,082,000,000 | 15 |
| ZRA | 675,601,261,068 | 845,979,000,000 | 25 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,196,242,240,068** | **1,446,061,000,000** | **21** |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA WASHIRIKA WA MAENDELEO | 634,426,593,000 | 1,416,517,992,000 | 123 |
| **JUMLA NDOGO** | **634,426,593,000** | **1,416,517,992,000** | **123** |
| **MAPATO YASIOKUWA YA KODI** | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 35,000,000,000 | ** | |
| KODI YA BOHARI | 1,065,399,000 | ** | |
| UHAMIAJI | 75,000,000,000 | 92,500,000,000 | 23 |
| UNUNUZI WA MAGARI | - | 25,000,000,000 | |
| **JUMLA NDOGO** | **111,065,399,000** | **117,500,000,000** | **6** |
| **MAPATO MENGINEYO YASIYOKUWA YA KODI** | | | |
| UUZAJI WA VIFAA VIKONGWE | 2,360,018,000 | ** | |
| KODI YA MAJENGO ZINAZOSIMAMIWA NA ORFM | 913,199,000 | ** | |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | 22,830,000 | 15,750,000 | - 31 |
| ADA YAMATUMIZI YA NYARAKA | 450,000,000 | 457,000,000 | 2 |
| MATANGAZO | 70,000,000 | 150,000,000 | 114 |
| USAJILI WA WAZABUNI | 180,000,000 | 300,000,000 | 67 |
| ADA YA MAFUNZO | 50,000,000 | 82,000,000 | 64 |
| **JUMLA NDOGO** | **4,046,047,000** | **1,004,750,000** | **- 75** |
| **JUMLA FO1** | **1,945,780,279,068** | **2,981,083,742,000** | 53 |
| **MAPATO FO4** | | | |
| VIBALI VYA UTAFITI | 64,750,000 | 78,650,000 | 21 |
| UKODISHWAJI WA KUMBI ZA MIKUTANO | 35,250,000 | 20,000,000 | - 43 |
| KUTOA USHAURI ELEKEZI JUU YA MASUALA YA TAFITI | 20,000,000 | 35,258,000 | 76 |
| **JUMLA FO4** | **120,000,000** | **133,908,000** | 12 |
| **MAPATO FO5** | | | |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI (PAYE) | 21,000,000,000 | 21,000,000,000 | - |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 8,400,000,000 | 10,000,000,000 | 19 |
| MABUKU NA STAKABADHI | 35,972,850 | 30,000,000 | - 17 |
| MCHANGO KUTOKA TAASISI YA VIWANGO (ZBS) | 2,400,000,000 | 2,500,000,000 | 4 |
| MCHANGO KUTOKA BPRA | 480,000,000 | 480,000,000 | - |
| MCHANGO KUTOKA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI | 1,920,000,000 | 2,000,000,000 | 4 |
| MCHANGO KUTOKA KAMISHENI YA UTALII | 4,800,000,000 | 5,000,000,000 | 4 |
| HATI FUNGANI | 150,000,000,000 | 180,000,000,000 | 20 |
| MKOPO KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO | 567,210,000,000 | 1,532,000,000,000 | 170 |
| GAWIO LA BOT | 13,500,000,000 | 13,500,000,000 | - |
| MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) | - | 2,500,000,000 | |
| MAMLAKA YA MAJI (ZAWA) | - | 3,750,000,000 | |
| MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) | - | 2,225,000,000 | |
| KAMISHENI YA ARDHI | - | 3,524,180,000 | |
| MISAADA YA KIBAJETI (GBS/URT) | 52,190,000,000 | 100,000,000,000 | 92 |
| MAPATO YATOKANAYO NA UENDESHAJI WA MASOKO | * | 6,005,500,000 | |
| **JUMLA FO5** | **821,935,972,850** | **1,884,514,680,000** | 129 |
| **MAPATO FO7** | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | *** | 33,701,170,000 | - |
| KODI YA BOHARI | *** | 470,000,000 | - |
| UUZAJI WA VIFAA VIKONGWE | *** | 1,365,012,000 | - |
| KODI YA MAJENGO ZINAZOSIMAMIWA NA ORFM | *** | 422,830,000 | - |
| **JUMLA FO7** | **-** | **35,959,012,000** | - |
| **JUMLA KUU** | **2,767,836,251,918** | **4,901,691,342,000** | 77 |
| | | | |
| **Angalizo** | | | |
| (-) : Taasisi hizi zitaanza rasmi kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2024/25 | | | |
| (*): Mapato ya Masoko yataanzwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 | | | |
| (**) : Mapato hayo kwa mwaka 2024/25 yanaonekana katika Fungu F07 | | | |
| (***) : Mapato hayo kwa mwaka 2023/24 yanaonekana katika Fungu F01 | | | |

*Jadweli Namba: 4 Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 (Tarakimu milioni)*

| Programu Kuu | Programu ndogo | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Miradi ya Maendeleo | | Ruzuku | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | Mhisani | | |
| Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | 668.74 | 644.45 | | | | 1,313.19 |
| | Marekebisho ya Mishahara | 130,665.10 | | | | | 130,665.10 |
| | Uratibu wa Fedha za Nje | 215.42 | 632.95 | | | | 848.37 |
| | Fedha na Sera za Kodi | 280.98 | 989.40 | | | 27,658.50 | 28,928.87 |
| | Jumla ndogo | **131,830.23** | **2,266.80** | **-** | **-** | **27,658.50** | 161,755.53 |
| Usimamizi wa Sera za Manunuzi na Masuala ya Sheria | Usimamizi wa Sera za Ununuzi | 804.17 | 322.36 | | | 2,953.50 | 4,080.03 |
| | Huduma za Kisheria za Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | | 358.66 | | | | 358.66 |
| | Jumla ndogo | **804.17** | **681.02** | | | **2,953.50** | 4,438.69 |
| Uendeshaji na uratibu wa wizara ya Fedha na Mipango | Utumishi na Uendeshaji | 1,334.29 | 31,055.75 | | | | 32,390.04 |
| | Mipango, Sera na Utafiti | 211.30 | 261.96 | 426,461.85 | 37,445.38 | | 464,380.49 |
| | Ofisi kuu Pemba | 591.21 | 1,837.00 | | | | 2,428.21 |
| | Jumla ndogo | **2,136.81** | **33,154.70** | **426,461.85** | **37,445.38** | | **499,198.74** |
| | **Jumla F01** | **134,771.20** | **36,102.52** | **426,461.85** | **37,445.38** | **30,612.00** | **665,392.95** |
| Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 2,791.90 | 414,105.50 | - | - | - | 416,897.40 |
| | Jumla ndogo | **2,791.90** | **414,105.50** | | | | 416,897.40 |
| | **Jumla F02** | **2,791.90** | **414,105.50** | | | | **416,897.40** |
| Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi | Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini | 256.41 | 216.89 | 3,000.00 | | | 3,473.30 |
| | Maendeleo ya Watendakazi wa Masuala ya Idadi ya Watu | 229.91 | 752.35 | | | | 982.26 |
| | Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo | 368.50 | 256.40 | 2,300.00 | | | 2,924.90 |
| | Jumla ndogo | **854.82** | **1,225.64** | **5,300.00** | | | 7,380.46 |
| Usimamizi wa Uchumi Mkuu | Usimamizi wa Uchumi Mkuu | 246.63 | 346.67 | | | | 593.30 |
| | Utafiti | 216.04 | 775.44 | | | | 991.48 |
| | Jumla ndogo | **462.68** | **1,122.10** | | | | 1,584.78 |
| Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | 659.54 | 1,619.46 | | | | 2,279.00 |
| | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Pemba | 311.77 | 210.57 | | | | 522.34 |
| | Jumla ndogo | **971.31** | **1,830.03** | | | | 2,801.34 |
| | **Jumla F03** | **2,288.80** | **4,177.77** | **5,300.00** | **-** | **-** | **11,766.57** |
| Kuendeleza na kuratibu Takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii | Ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii | 1,059.58 | 945.92 | | 5,345.24 | | 7,350.73 |
| | Uratibu wa shughuli za Kitakwimu katika mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar | 277.87 | 186.02 | | 1,117.88 | | 1,581.77 |
| | Jumla ndogo | **1,337.45** | **1,131.94** | **-** | **6,463.12** | **-** | 8,932.50 |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Utawala na Uendeshaji Unguja | 684.80 | 822.26 | | 2,199.25 | | 3,706.32 |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba | 329.75 | 145.00 | | | | 474.75 |
| | Jumla ndogo | **1,014.55** | **967.26** | | **2,199.25** | | 4,181.07 |
| | **Jumla F04** | **2,352.00** | **2,099.20** | **-** | **8,662.37** | **-** | **13,113.57** |
| Usimammizi wa Hazina | Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali yasiyokuwa ya Kodi | | 58.36 | | | | 58.36 |
| | Kusimamia ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali | | 213.38 | | | | 213.38 |
| | Usimamizi wa Matumizi ya Serikali | | 552.53 | | | | 552.53 |
| | Usumamizi wa Deni la Taifa | | 266.12 | | | | 266.12 |
| | Jumla ndogo | | **1,090.38** | | | | 1,090.38 |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Uratibu wa Mipango | | 101.17 | | | | 101.17 |
| | Utawala na Uendeshaji Unguja | 8,626.79 | 1,681.31 | | | | 10,308.09 |
| | Utawala na Uendeshaji Pemba | 2,751.01 | 503.34 | | | | 3,254.36 |
| | Jumla ndogo | **11,377.80** | **2,285.82** | | | | 13,663.62 |
| | **Jumla F05** | **11,377.80** | **3,376.20** | | | | **14,754.00** |
| Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali | Usimamizi wa kamati za Ukaguzi na Taarifa jumuishi za ukaguzi wa ndani | | 142.12 | | | | 142.12 |
| | Uchunguzi wa Ubadhirifu na vihatarishi | | 397.84 | | | | 397.84 |
| | Usimamizi wa uthibitisho wa ubora | | 285.34 | | | | 285.34 |
| | Jumla ndogo | | **825.29** | | | | 825.29 |
| Utawala na Uendeshaji | Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango,Mafunzo na Utafiti | 3,365.87 | 788.33 | | | | 4,154.20 |
| | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Ofisi Pemba | 848.14 | 241.88 | | | | 1,090.01 |
| | Jumla ndogo | **4,214.00** | **1,030.21** | | | | 5,244.21 |
| | **Jumla F06** | **4,214.00** | **1,855.50** | **-** | **-** | **-** | **6,069.50** |
| Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya | Usimamizi wa mali za Umma | 151.60 | 562.03 | | | | 713.63 |
| | Uwekezaji wa Mashirika ya Umma | 303.20 | 2,350.55 | | | | 2,653.75 |
| | **Jumla ndogo** | **454.80** | **2,912.58** | | | | **3,367.38** |
| Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina | Usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina | 329.10 | 962.79 | | | | 1,291.90 |
| | Uratibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Pemba | 152.10 | 407.13 | | | | 559.23 |
| | Jumla ndogo | **481.20** | **1,369.92** | **-** | **-** | **-** | 1,851.13 |
| | **Jumla F07** | **936.00** | **4,282.50** | | | | **5,218.50** |
| | **JUMLA KUU** | **158,731.70** | **465,999.19** | **431,761.85** | **46,107.75** | **30,612.00** | **1,133,212.49** |

*Jadweli Namba: 5 Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 (Tarakimu Milioni)*

| S/ N | PROGRAMU/ MIRADI | WASHIRIKA WA MAENDELEO | FEDHA ZA SMZ | MKOPO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Fungu F01** | | | | |
| 1 | **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | |
| | Ukamilishwaji wa Ofisi za Serikali | | 80,261.187 | | 80,261.187 |
| | Ujenzi wa Mji wa Serikali | | 33,722.161 | | 33,722.161 |
| | **Jumla ya programu ya ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | **113,983.348** | | **113,983.348** |
| 2 | Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha ( PFMRP) | Benki ya Dunia | 400.000 | 4,458.506 | 4,858.506 |
| 3 | Uimarishaji wa Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISPDRM) | Benki ya Maendeleo ya Afrika | 78.500 | 986.878 | 1,065.378 |
| 4 | Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar ( BIG-Z) | Benki ya Dunia | | 32,000.000 | 32,000.000 |
| 5 | Ulipaji wa Mdeni kwa Miradi ya Maendeleo | | 312,000.000 | | 312,000.000 |
| | **Jumla F01** | | **426,461.848** | **37,445.38** | **463,907.232** |
| | **F03** | | | | |
| 6 | Mradi wa Mapitio, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wa Mpango wa maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, VISION 2050, SDGs na AFRICAN AGENDA) | | 2,300.000 | | 2,300.000 |
| 7 | Kuratibu Mpango wa Kurasimisha Ardhi na Biashara Zanzibar | | 3,000.000 | | 3,000.000 |
| | **Jumla F03** | | **5,300.000** | | **5,300.000** |
| | **F04** | | | | |
| 8 | Mradi wa Uendelezaji Takwimu (ZSDP) | Benki ya Dunia | | 8,662.367 | 8,662.367 |
| | **Jumla F04** | | | **8,662.37** | **8,662.367** |
| | **JUMLA KUU** | | **431,761.848** | **46,107.751** | **477,869.599** |